# Nipashe

Jumanne Septemba 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580325

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Kamati Kuu CCM yateua majina wagombea uwakilishi Zanzibar

UKURASA 3



Nipashe

TESA

Jumanne Septemba 1, 2020

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

KITIKHO MYOTO

Kilimo, radi, kisangazi vyatajwa kuleta balaa

SAYANSI NA AGNES TEMU

Biashara mtandaoni Kinamama watoboa kipindi cha corona

RUFIJI NI MAAJABU

Umeficha mji uliozama, wataalamu kuujenga upya

UKURASA 11

# ACT-Wazalendo yataja vipaumbele muhimu 11

## **YAAHIDI** elimu bure hadi chuo kikuu, bima ya afya kwa kila Mtanzania... *Endelea uk. 2*



Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (katikati), akiwa na mgombea urais kupitia chama hicho, Bernard Membe (kulia) na mgombea mwenza, Prof. Omary Kakhi Mohammed, wakionyesha ilani ya uchaguzi, baada ya kuizindua, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Askofu KKKT akerwa na matusi kampeni uchaguzi

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**WAGOMBEA URAIS ZANZIBAR WAFIKIA 15**
IDADI ya wagombea urais Zanzibar imezidi kuongezeka na kufikia...

**UKURASA WA 4**

**RUGWE KUZINDUA KAMPENI, AAHIDI KUWAPO UBWABWA**
MGOMBEA urais wa Chama cha CHAUMMA, Hashimu Rugwe, amesema atazindua kampeni zake....

**UKURASA WA 5**

**WATUMISHI TPA, MKANDARASI KORTINI**
TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imewafikisha mahakamani watu watano wakiwamo...


## BODI YA MIKOPO YAONGEZA MUDA WA MAOMBI

UKURASA 5

**MICHEZO** SVEN AKUNWA NA MAJEMBE YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mgombea urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwapungia mkono wakazi wa Jiji la Arusha jana, alipowasili katika viwanja vya Relini kwa ajili ya kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mambo 11 muhimu ilani ya ACT

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimezindua ilani yake ya uchaguzi wa mwaka huu, kikibainisha mambo 11 muhimu kiliyopanga kuyatekeleza iwapo kikishinda kuongoza nchi.

Chini ya mgombea wake wa urais, Bernard Membe, chama hicho kimeweka kipaumbele katika masuala ya haki za uhuru na demokrasia, elimu, afya, uvuvi, kilimo, mifugo, michezo, sanaa na uhusiano wa kimataifa.

Wakati wa uzinduzi wa ilani hiyo jijini Dar es Salaam jana, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alianza kwa kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa mwaka 2015-2025), akidai utekelezaji wake haujamridhisha.

Kwa kuzingatia hilo, Zitto alisema chama chao kimetengeneza ilani ambayo kinaamini utekelezaji wake utakuwa tiba kwa matatizo lukuki yanayowakabili wananchi, ukiwamo ukosefu wa ajira.

**UHURU, DEMOKRASIA**

Katika ilani hiyo ya ACT-Wazalendo, eneo la kwanza lililopewa kipaumbele ni uhuru, haki na demokrasia, chama hicho kikiahidi kuwa kitafuta sheria kilizoziita kandamizi uhuru wa watu na demokrasia.

Sambamba na hilo, chama hicho pia kimeahidi kuunda tume ya majaji ili kuchunguza matukio makubwa yaliyotokea nchini hivi karibuni, yakiwamo yanayodaiwa kufanywa na watu wasiojulikana.

**TAKUKURU, CAG**

Kupitia ilani hiyo, ACT-Wazalendo pia imesema itaangazia suala la uwajibikaji kwa kuimarisha taasisi za kusimamia uwajibikaji kama vile Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliyo chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Mamlaka ya Mapato (TRA) ili kuwajibika kwa ufanisi zaidi.

**KATIBA MPYA**

Kama ilivyo kwa vyama vya upinzani vya CHADEMA na CUF, hoja ya Tanzania kuandaa katiba mpya imegusiwa pia kwenye ilani hiyo ya ACT-Wazalendo, chama hicho kikiahidi kuufufua mchakato wa katiba mpya ili kuukamilisha na kuhakikisha wananchi wanapata katiba inayoendana na mahitaji ya sasa.

**ELIMU BURE CHUO KIKUU**

Wakati chama kinachoongoza serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kikijivunia mafanikio ya mpango wake wa kutoa elimumsingi bila malipo kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne, ACT-Wazalendo kimeahidi kuwa kikishika dola, elimu itatolewa bure hadi ngazi ya chuo kikuu.

Katika uzinduzi wa ilani hiyo jana, chama hicho kiliahidi kuwa kitaboresha mfumo wa elimu kwa wanafunzi kusoma bure kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu, gharama zikitakiwa kubaki kwa serikali.

Sambamba na hilo, chama hicho kiliahidi kuwa kitaifuta mikopo yote ya wanafunzi wa elimu ya juu katika siku ya kwanza tu kazini Ikulu ya rais kupitia chama hicho na serikali italazimika kuandaa mfumo mpya wa kugharamia elimu ya juu na vyuo vya ufundi.

**BIMA KWA KILA RAIA**

Kwenye sekta ya afya, chama hicho kimeahidi kuweka mfumo wa afya utakaohakikisha kila mwananchi anakuwa na bima ya afya itakayomwezesha kupata matibabu kwa gharama nafuu huku pia kikiahidi kuongeza idadi ya hospitali na zahanati nchini sambamba na wahudumu wa afya, ili kuhakikisha kila daktari mmoja anatibu wagonjwa 1,000 inavyotakiwa kisera.

**TRIL.10/- ZA MAJI**

Kuhusu sekta ya maji, chama hicho kimeahidi kuwekeza Sh. trilioni 10 katika miundombinu ya maji ili kumaliza kero za maji nchini, kikibainisha kuwa kitahakikisha hilo linawezekana kwa kutenga wastani wa Sh. trilioni mbili kwa mwaka.

**KILIMO, MIFUGO, UVUVI**

Kupitia ilani hiyo, ACT-Wazalendo pia kimeahidi kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuanzisha kile walichoita kilimo cha kimapinduzi kupitia ushirika wa kisasa na pia kuanzisha skimu ya hifadhi ya jamii kwa wakulima, wavuvi na wafugaji.

**SEKTA BINAFSI**

Vilevile, chama hicho kimeahidi kuwa kitaweka mazingira wezeshi kama vile sera na sheria nzuri na rafiki kwa uwekezaji zinazotabirika na zisizobadilika badilika ili kutokuleta mkanganyiko kwa wawekezaji.

MIRADI MIKUBWA

Kupitia ilani hiyo, ACT-Wazalendo kimeahidi kusimamia miradi saba ya kimkakati, ikiwamo ya Mchuchuma na Liganga, uchimbaji madini ya Nikeli katika eneo la Kabanga wilayani Ngara mkoani Kagera na kusimamia uwekezaji wa eneo la kiuchumi la Bagamoyo.

Pia, kuimarisha Bandari ya Mtwara, kurejesha Mradi wa Gesi Asilia (LNG Plant) kwa kuharakisha mazungumzo na wawekezaji na kuondoa vikwazo vyote na nchi kuwa mzalishaji mkubwa wa gesi barani Afrika.

**MICHEZO, SANAA**

ACT-Wazalendo pia kimeahidi kuweka mazingira rafiki katika sekta ya michezo itakayowainua wasanii kiuchumi na kuliwezesha taifa kupata mapato ya kutosha kupitia sekta hiyo.

**DIPLOMASIA**

Eneo la 11 lililopewa kipaumbele katika ilani hiyo ni uhusiano wa kimataifa, chama hicho kikiahidi kuboresha uhusiano wa kimataifa kati ya Tanzania na mataifa mengine ili kunufaika kiuchumi na kidiplomasia. Mgombea urais wa Tanzania kupitia chama hicho, Membe alifafanua kaulimbiu yao ya 'Kazi na Bata', akisema inamaanisha kufanya kazi yenye kipato kizuri, kwa tija na kupata muda wa mapumziko na furaha kwa anayefanya kazi.

Katika uzinduzi wa ilani hiyo, Membe pia alizungumzia masuala kadhaa ya kisiasa, kiuchumi na kidiplomasia na kutoa sababu ya kutokwenda mahakamani kumshtaki aliyedukua mawasiliano yake ya simu, akidai kuwa ni kutokana na wasimamizi wa sheria kutolitia mkazo suala hilo.

Membe, ambaye alijiunga na ACT-Wazalendo Julai mwaka huu baada ya kutimuliwa uanachama wa CCM, alisema kuwa leo wanatarajia kuzindua rasmi kampeni za chama chao mkoani Lindi.

## Askofu KKKT akemea matusi kwenye kampeni, aonya rushwa

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WITO umetolewa kwa wanasiasa wote nchini kufanya siasa za kistaarabu na kuepuka rushwa na matusi katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Morogoro, Jacob ole Mameo, alitoa wito huo juzi wakati wa ibada ya ufunguzi wa nyumba ya mchungaji wa kanisa hilo, Usharika wa Lungo, Mvomero mkoani Morogoro.

Askofu Mameo aliwataka wanasiasa na mashabiki wa siasa kote nchini kuitunza amani ya nchi kwa kuepuka vurugu, matusi na rushwa kwenye majukwaa ya kampeni.

"Tunawaomba wanasiasa wafanye kampeni zao kistaarabu, waseme sera zao na waache kutukana, maana matusi na vurugu sio sera... waseme kile wanachotaka kuwafanyia Watanzania," alisema Askofu Mameo.

Askofu Mameo aliongeza kuwa kwa miaka mingi Tanzania imekuwa kisiwa cha amani, hivyo kila mmoja anapaswa kuendelea kuitunza amani hiyo kwa kuepuka vitendo vyovyote vinavyoweza kuchochea vurugu na uvunjifu wa amani.

Akizungumzia kuhusu rushwa, Askofu Mameo alisema kuwa wanasiasa waepuke kutoa rushwa kwa kuwa rushwa hupofusha macho, na huondoa uwezo wa kufikiri vema.

"Kiongozi akiwapa rushwa watu ili wamchague huwafanya watu hao kuchagua pasipo umakini. Rushwa ni adui wa haki, kuchagua au kuchaguliwa kwa misingi ya rushwa huwaondolea watu haki ya kupata kiongozi bora," alisema Askofu Mameo na kuongeza:

"Wanasiasa ambao huendekeza rushwa, acheni kutoa rushwa kwa lengo la kushawishi kuchaguliwa. Wanaotoa na kupokea rushwa wanapaswa kutubu kwa kuwa rushwa ni dhambi kubwa, ambayo inapaswa kuepukwa kwa kila namna."



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, akiongoza kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Wagombea uwakilishi CCM Zanzibar hadharani

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imepitisha majina 50 ya wanachama watakaogombea ujumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole alisema Kamati Kuu ya CCM iliketi mjini Dodoma ikiwa ni mwendelezo wa kuelekea uchaguzi mkuu.

"Ni uteuzi wa mwisho wa wanachama wa CCM wa kugombea Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Kamati Kuu imejadili, imetafakari na kuwateua watu hodari na mabingwa katika uongozi," alisema.

"Ni watu ambao Zanzibar ipo mikononi mwao katika kuwaletea maendeleo, wameteuliwa watu ambao wakilala na kuamka wataleta mawazo ya kuijenga Zanzibar, Wawakilishi ambao wanasadifu maono ya mgombea urais wa Zanzibar," aliongeza.

Polepole aliwataja waliopitishwa na majimbo kwenye mabano kuwa ni Zawadi Aamour Nasoro (Konde), Shamata Shahama Khamisi (Micheweni), Saidi Sale Salim (Tumbe), Tunu Mwalimu Masoud (Wingwi), Maliam Dhani Juma (Gando), Makame Said Juma (Kojani) na Othman Ali Khamis (Mtambwe).

Wengine ni Khamis Dadi Khamis (Pandani), Harus Said Suleiman (Wete), Shaibu Hassan Kaduara (Chake) Suleiman Masoud Makame (Chonga) Masoud Ali Mohammed (Ole), Bakari Hamad Bakari (Wawi), Suleiman Makame Ali (Ziwani), na Bahati Khamis (Chambani).

Mussa Kombo Mussa (Kiwani), Abdul Hussein Kombo (Mkoani), Mohammed Mgaza Jecha (Mtambile), Nadir Yussuf (Chaani), Juma Mkungu Juma (Kijini) na Mkwajuni ni Sulubu Kidongo Amour.

Pia wamo Abdul Abbas Wadi (Nungwi), Haji Omar Kheri (Tumbatu), Mtumwa Peya Yussuf (Bumbwini), Khalid Salum Mohammed (Donge), Asha Abdallah mussa (Mahonda), -Issa Haji Gavu (Chwaka), Haroun Ali Suleiman (Makunduchi), Paje- Dk. Soud Nahoda Hassan (Paje) na Mwanaasha Khamis Juma (Dimani).

Wengine ni Yussuf Hassan Iddi (Fuoni), Suleiman Haroub Suleiman (Kiembe Samaki), Ameir Abdallah Ameir (Mwanakerekwe), Ali Suleiman Ameir (Pangawe), Mudrik Ramadhan Soraga (Bububu), Machano Othman Said (Mfenesini), Hussein Ibrahim Makungu (Mtoni), Mihayo Juma Nhunga (Mwera), Hassan Khamis Hafidh (Welezo) na Rukia Omar Mapuri (Amani).

Miraji Khamis Mussa (Chumbuni), Jamaal Kassim Ali (Magomeni), Shaaban Ali Othman (Mpendae), Hamza Hassan Juma (Shaurimoyo), Ali Gullam Hussein (Jang'ombe), Nassor Salum Ali (Kikwajuni), Yahya Rashid Abdallah (Kwahani) na Malindi ni Mohammed Ahmada Salum

Polepole alisema Kamati Kuu imepitisha majina ya wawakilishi kundi la wanawake kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba ambao ni Bihindi Hamadi Khamis, Chumu Kombo Khamis, na Farida Hamad Juma na Kaskazini Unguja ni Panya Ali Abdalah, Mwanajuma Kasim Makame na Fatma Hamza Mohamed.

Mkoa wa Kusini Pemba waliopitishwa ni Shadia Mohamed Suleimani, Zuhura Mgeni Othman na Zainab Omar Amir wakati Mkoa wa Kusini Unguja ni Salma Juma Bilal, Rahma Kasim Ally na Arafa Ali Yusuph.

Katika mkoa wa Magharibi Unguja, waliopitishwa ni Fatma Ramadhani Mandoba, Mwanaidi Kassim Mussa na Fatma Ali Akhmed na Mkoa wa Mjini Magharibi ni Saada Ramadhani Mwendwa, Mgeni Hassan Juma na Salma Abdi Ibada.

Kadhalika, Polepole alisema Kamati Kuu imewapitisha wawakilishi wanawake kwenye kundi la wenye ulemavu, ambao ni Mwantatu Mbaraka Khamis na Zainab Abdallah Salum na kundi la wasomi ni Riziki Pembe Juma,

Kwenye kundi la Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) waliopitishwa ni Salha Mohamed Mwinjuma na Rahma Mbaraka Tahir na kwa upande wa wazazi ni Sabiha Filfili na Aza Januari Joseph.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA JUU YA KUSUDIO LA KUFUTA LESENI

**(Imetolewa chini ya Kanuni ya. 21 (2) ya Kanuni za Petroleum (Jumla, Hifadhi, Rejareja na Miundombinu ya Kuhifadhia Mafuta kwa matumizi Binafsi), Toleo la Na. 380 la Gazeti la Serikali la 2018)**

**TAARIFA inatolewa kwa umma kuhusu kusudio la EWURA la kufuta leseni Na. PWL-2019-002 ya uendeshaji biashara ya mafuta kwa ujumla ya Kampuni ya Multimodal Petroleum Africa Limited,** yenye ofisi zake **Jengo Na. 121, Kiwanja 8/1, Mtaa wa Nkurumah; Eneo la Gerezani, Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam.** Kusudio hili linatokana na Kampuni hiyo kushindwa kufanya biashara ya mafauta kwa jumla **(kutoagiza bidhaa za mafuta)** kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita (6), kinyume na masharti ya leseni na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Petroli **(Jumla, Hifadhi, Rejareja na Miundombinu ya Kuhifadhia Mafuta kwa matumizi Binafsi),** Toleo Na. 380 la Gazeti la Serikali la Mwaka 2018.

**Vinginevyo,** Kampuni hiyo iwasilishe **ndani ya siku 21 tangu taarifa hii kutolewa,** maelezo yanayokubalika na kujitosheleza kisheria; kwa nini leseni yake isifutwe. Baada ya hapo, EWURA itaendelea na utaratibu wa kufuta leseni hiyo pasipo kutoa taarifa nyingine.

**Imetolewa Na:**

**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI – EWURA**
**01 Septemba, 2020**

# Wagombea urais Zanzibar wafikia 15

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

IDADI ya wagombea urais Zanzibar imezidi kuongezeka na kufikia 15 hadi sasa.

Jana, wagombea wengine wawili walichukua fomu ya kugombea urais wa Zanzibar na kukabidhiwa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, katika ofisi za tume hiyo, Maisara mjini Zanzibar.

Majira ya saa 8:30 mchana, mgombea wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), Hussein Juma Salim, alifika ZEC kuchukua fomu na wakati akizungumza na waandishi wa habari aliahidi kuwa ataboresha sekta ya elimu iwapo atapata ridhaa ya kuongoza Zanzibar.

Pia alisema endapo atachaguliwa atahakikisha anaboresha maslahi ya walimu ili wafundishe vizuri na kuongeza ufaulu.

"Kila mwaka matokeo ya taifa ya wanafunzi wetu wa sekondari Zanzibar si mazuri ikilinganishwa na Tanzania Bara. Nitahakikisha walimu wanapata stahiki zao na kuongeza mshahara kwa wafanyakazi wote," alisema.

Pia alisema ataimarisha uchumi wa Zanzibar ili kupata maendeleo na kumpongeza Rais anayemaliza muda wake, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa jitihada zake za kuiletea maendeleo Zanzibar.

Sambamba na hilo, alisema ataongeza kiwango cha mishahara na kwamba kima cha chini kitakuwa Sh. 600,000 badala ya Sh. 300,000.

Hata hivyo, alisema yuko tayari kukubali matokeo ya uchaguzi mkuu endapo atashindwa.

Naye mgombea wa Chama cha UMD, Mohamed Omar Baharia, aliyefika ZEC majira ya saa 9:30 alasiri, endapo atapata ridhaa, vipaumbele vyake ni kukuza ajira hasa kwa vijana.

Aidha, alisema atadumisha amani ya nchi na hatakuwa tayari kuona mtu yeyote anaivuruga na kwamba atahakikisha anakuza sekta ya uchumi hasa katika eneo la bahari na kilimo cha karafuu.

"Nataka uchumi wa bahari kuutumia ipasavyo na kuwa na viwanda vikubwa ambavyo vitakua vinatumia mazao ya bahari kuimarisha uchumi," alisema.

Akiwakabidhi fomu wagombea hao, Jaji Hamid aliwataka kuzingatia kanuni na maadili ya uchaguzi ikiwamo kutojihusisha na rushwa.

Wagombea 15 waliochukua fomu hadi jana ni Dk. Hussein Mwinyi (CCM), Said Soud (AAFP), Juma Ali Khatib (ADA-TADEA), Hamad Rashid (ADC) , Mfaume Khamis (NLD), Ali Juma (CHAUMA), Issa Muhammed Zonga (SAU), Ameir Said Ameir (Demokrasia Makini) na Hamad Muhammed Ibrahim (UPDP).

Wengine ni Shafii Hassan Suleiman (DP), Khamis Faki Mgau (NRA), Maalim Seif Sharif Hamad (ACT Wazalendo), Othman Rashid Khamis (CCK), Hussein Juma Salim na Mohamed Omar Baharia.



Mgombea wa urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Tanzania Labour (TLP), Hussein Juma Salim (kulia), akipokea fomu ya uteuzi wa nafasi hiyo, kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watumishi wa umma waonywa kuwa na mihemko ya kisiasa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WATUMISHI wa umma wametakiwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na kujiepusha na mihemko ya kisiasa katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Dk. Fransis Michael, alisema hayo jana katika kikao cha tathmini ya utendaji kazi kwa watendaji wa Wizara ya Maji, kilichofanyika jijini hapa.

Alisema kuna sheria na kanuni zinazomkataza mtumishi wa umma kwenye masuala ya kisiasa ikiwamo kutumia nafasi yake kwa manufaa yake au kupendelea mtu fulani.

"Tunaelekea kwenye kipindi cha uchaguzi, lazima tujue majukumu yetu nini. Sisi kama watumishi wa umma, hilo lazima kila mtumishi kulitambua bila kusahau uadilifu," alisema.

Aidha, alisema watumishi wa umma wana haki ya kidemokrasia kuchagua na kuchaguliwa au kuwa mwanachama wa chama fulani cha siasa nchini.

"Mtumishi wa umma kushiriki katika masuala ya siasa katika vyama inaruhusiwa ila tu wasipendelee mtu kwa kuwa mtumishi huyo au watumishi hao watakuwa na mapenzi na chama fulani cha siasa," alisema.

Katika masuala ya siasa, alisema mtumishi wa umma hana budi kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa za utumishi wa umma na utawala bora.

Naye Naibu Mwanasheria Mkuu Serikali, Dk. Evaristo Longopa, alisema ibara ya 113(a) inakataza majaji na mahakimu kujiunga na chama chochote cha siasa kwa sababu wenyewe ndio watoa haki.

Akifungua kikao hicho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, aliwataka watendaji wa idara za maji kufanya kazi kwa ushirikiano ili wananchi wapate huduma hiyo kwa uhakika.

Sanga alisema kuna baadhi ya watendaji wanafanya kazi bila ushirikiano hali ambayo inapunguza tija katika kutoa huduma hiyo. Aliwaagiza wakurugenzi wote katika idara za maji kuimarisha utendaji kazi.

"Maeneo mengi bado kuna umimi. Naomba umimi huu tuumalize, tushirikiane katika utendaji wetu kwa ajili ya kufanya kazi yetu iwe bora zaidi katika kuwatumikia wananchi," alisema.

"Kila mmoja naomba ajiulize maswali matatu. Je, katika eneo langu wananchi wanapata huduma bora ya maji? Kama hawapati kuna mradi gani ninautekeleza? Na kama hakuna mradi, mpango gani upo?" Alisisitiza.

# Rugwe kuzindua kampeni, aahidi kuwapo ubwabwa

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA urais wa Chama cha CHAUMMA, Hashimu Rugwe, amesema atazindua kampeni zake Septemba 5, mwaka huu katika viwanja vya Manzese, Dar es Salaam.

Aidha, amesema wananchi wasikose kwenda kwenye uzinduzi huo kwa kuwa kutakuwa na chakula cha kutosha kwa kila atakayekwenda.

Rungwe aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kwa simu kuhusu uzinduzi wa kampeni zake na uwapo wa ubwabwa kama ambavyo amesikika akiahidi mara kwa mara.

Alipoulizwa kuhusu uzinduzi wa ilani ya chama hicho, alisema: "Ilani ya chama itazunduliwa siku hiyo katika mkutano. Tutaweka wazi vipaumbele vyetu, wananchi waje kwa wingi bila kukosa.

"Watu waje kwa wingi kutakuwa na mapishi kwa wingi, ninachosisitiza watu waje kama kuna chakula watakiona baada ya kufika," alisema.

Rugwe alikaririwa akisema serikali atakayoiunda itahakikisha inagawa wali kwa wanafunzi shuleni, ili kuwawezesha kusoma na kufaulu vyema.

Mwanasiasa huyo ni miongoni mwa wagombea 17 waliopitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Agosti 25, mwaka huu, na baadhi wameshazindua kampeni za vyama vyao katika ngazi ya urais.

**Rungwe aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kwa simu kuhusu uzinduzi wa kampeni zake na uwapo wa ubwabwa kama ambavyo amesikika akiahidi mara kwa mara.**

# Watumishi wa TPA, mkandarasi kortini

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imewafikisha mahakamani watu watano wakiwamo watumishi wanne wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kwa tuhuma za rushwa, uhujumu uchumi na ukwepaji kodi wa Sh. milioni 153.5.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Ofisa Uhusiano wa TAKUKURU, Doreen Kapwani, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, ilieleza kuwa watumishi hao wa TPA walishafukuzwa kazi.

Alisema mtumishi mmoja ni Mkurugenzi wa Kampuni ya M/S Saxon Building Contractors Limited iliyopewa zabuni ya ujenzi wa gati la Sibwesa katika Ziwa Tanganyika.

Kapwani alisema TAKUKURU bado inaendelea kumtafuta mtuhumiwa mwingine aliyekuwa Mhasibu wa Bandari ya Kigoma, Madaraka Robert, ili kuunganishwa kwenye kesi hiyo.

Alitaja majina ya watuhumiwa hao ambao walifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kigoma jana kuwa ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Saxon Building Contractors Limited, Rodrick Uisso na aliyekuwa Meneja wa Bandari ya Kigoma, Ajuaye Msese.

Wengine ni aliyekuwa Ofisa Mhasibu wa TPA Kigoma, Herman Shimbe na aliyekuwa Mhandisi Mkazi wa TPA Kigoma, Jesse Mpenzile.

Kapwani alisema uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU ulibaini kuwa washtakiwa hao walihusika kutenda makosa ya rushwa na uhujumu uchumi yakiwamo ya kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo, ukwepaji kodi, kuisababishia mamlaka hasara na utakatishaji fedha haramu.

"Sambamba na kuwafikisha watuhumiwa hao watano mahakamani leo (jana), uchunguzi huu wa TAKUKURU bado utaendelea kwa lengo la kubaini kiasi kingine cha fedha zilizohujumiwa ikiwa ni pamoja na kumtafuta Madaraka Robert aliyehusika katika tuhuma hizo ili aunganishwe katika shauri hili," alisema Kapwani.




Kiongozi wa Waislamu Shia Ithnasheriya, Sheikh Hemed Jalala (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, katika maadhimisho ya Siku ya Ashura yaliyoambatana na matembezi ya amani, yaliyoanzia katika viwanja vya Ilala Boma na kuishia Kigogo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# HESLB yaongeza muda wa kuomba mikopo

**Na Halfan Chusi**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imetangaza kuongeza muda wa siku 10 za kuomba mkopo kuanzia leo, ili kuwawezesha wanafunzi ambao hawajakamilisha maombi yao kukamilisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa uamuzi huo unafuatia maoni, ushauri na maombi kutoka kwa wanafunzi, wazazi na walezi ambayo bodi imeyapokea.

"Hadi leo (jana) asubuhi, tumeshapokea maombi 85,921 kwa njia ya mtandao. Kati ya hayo, maombi 71,888 sawa na asilimia 84 ni kamilifu na yana nyaraka muhimu na mengine 14,033 yanakosa nyaraka muhimu kama vyeti vya kuzaliwa au vya vifo vya wazazi wa waombaji ambavyo havijathibitishwa na RITA au Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA)," alisema.

Badru aliongeza HESLB imeendesha programu za elimu ya uombaji mkopo kwa usahihi kwa wanafunzi katika mikoa 14 ya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na kwenye kambi 18 za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambako wamepokea maoni na maombi ya kuongezwa kwa muda ili kutoa nafasi kwa wanafunzi walioko kwenye kambi za JKT kuomba mkopo mara wamalizapo mafunzo.

"Kuhusu waliopo JKT hivi sasa, tunaendelea kuwasiliana na makao makuu ya JKT ambao tunashirikiana kuhakikisha vijana wote wahitaji wanapata fursa bila kuathiri mafunzo ambayo ni muhimu," alisema Badru.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa katika mwaka wa masomo 2020/2021, serikali imetenga Sh. bilioni 464 kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi 145,000 wa taasisi za elimu ya juu. Kati yao, 54,000 wanatarajiwa kuwa ni wa mwaka wa kwanza.

"Hili ni ongezeko la kutoka jumla ya Sh. bilioni 450 zilizotolewa mwaka huu (2019/2020) ambazo zimewanufaisha jumla ya wanafunzi 132,292 hadi sasa," al;isema Badru katika mkutano huo uliohudhuriwa pia na wawakilishi kutoka RITA na Shirika la Posta Tanzania (TPC), taasisi zinazowahudumia waombaji mkopo.

Katika mkutano huo, Meneja Masoko wa Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (RITA), Josephat Kimaro, aliwakumbusha wanafunzi waombaji mkopo waliowasilisha maombi ya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa au vya vifo vya wazazi wao, kufungua barua pepe walizotumia kuwasilisha maombi yao RITA ili kupokea majibu.

Meneja Mkuu anayesimamia Uendeshaji Biashara wa TPC, Mwanaisha Said, alisema wamekubaliana na HESLB kuendelea kupokea nakala ngumu za maombi ya mikopo katika ofisi za TPC nchini kote na kuziwasilisha HESLB hadi Septemba 15 na kuwataka wanafunzi kutokuwa na wasiwasi na kutokupokewa kwa bahasha zao.

## Viongozi vijana waonywa ujuaji

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imewataka viongozi vijana kuacha tabia ya kujiona kila kitu wanakijua katika ofisi, hivyo kuharibu taasisi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), Dk. Laurean Ndumbaro, wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya uongozi ngazi ya cheti yanayotolewa na Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto Executive Education cha Finland.

Alisema viongozi hao waache tabia ya kujiona wanaelewa, badala yake wajishushe ili waweze kupatiwa ushauri.

"Hii ni changamoto, lazima ujishushe ili uende na wananchi mfano, viongozi wengi vijana wameteuliwa, kuna taasisi moja inaongozwa na vijana na wasaidizi wake ni vijana, lakini anashangaa kwa nini yeye haeleweki kwa wenzake wanamshangaa kwa nini haeleweki."

Aliongeza: "Kumekuwa na mgogoro katika hii ofisi na watumishi wengi wanaingia na kutoka kwa sababu ni yeye anajiona anaelewa kila kitu... huko sio kujiamini ni kuharibu, ukiwa kama kiongozi unatakiwa kuliangalia hilo kwa kuwa tabia hiyo huwafanya baadhi ya watu kushindwa kukushauri."

Alisema kiongozi mzuri anapaswa kujishusha na muda wote awe mtu wa kujifunza ili iwe rahisi watu wengine kufika ofisini kwake na kumshauri.

Dk. Ndumbaro alisema kiongozi anapaswa kujiamini kwa kutambua changamoto zilizopo, ambazo zinazunguka jamii ambayo anaiongoza badala ya kujifanya ni mjuaji wa kila kitu.

Naye Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Uongozi, Prof. Penina Mlama, alisema bado nchi inakabiliwa na changamoto ya wanawake kushika nafasi za chini za uongozi, hivyo ni wajibu wa vijana kushirikiana kuhakikisha wanatatua tatizo hilo.

"Tutaweza kulitatua jambo hilo kama wanawake waliopata nafasi za uongozi watatoa fursa kwa wenzao ili kuwapo na uwiano sawa," alisema.

Awali akifungua mafunzo hayo, Katibu Mkuu Ikulu, Dk. Moses Kusiluka, alisema programu hiyo ni ishara ya kuunga juhudi za maendeleo nchini na kuimarisha uwezo wa viongozi inayofanywa na Taasisi ya Uongozi kuimarisha utawala bora.

"Nimefahamishwa kwamba programu za mafunzo kwa viongozi zinazoandaliwa na kutolewa na Taasisi ya Uongozi zinalenga kuimarisha uwezo wa viongozi katika maeneo matatu:

Kufanya maamuzi ya kimkakati, kuongoza rasilimali watu na rasilimali nyingine na kujenga sifa binafsi za kiongozi," alisema.

Naye Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema mafunzo hayo ni programu ya miezi sita yenye moduli tatu na yanawalenga viongozi chipukizi na waandamizi wanaofanya kazi katika taasisi mbalimbali barani Afrika.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Vyama vinavyoshiriki uchaguzi vihakikishe vinawafikia Watanzania

VYAMA kadhaa vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu vilizindua rasmi kampeni zao na kuanza mikutano ya kampeni maeneo mbalimbali.

Vyama ambavyo vilizindua kampeni hizo kitaifa ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambacho kilizindua kampeni zake Ijuaa jijini Dar es Salaam na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jumamosi jijini Dodoma.

Baadhi ya vyama kama ACT-Wazalendo kimesema kuwa kitazindua kampeni zake mkoani Lindi wakati Chama cha Wananchi (CUF) kimeahidi kuzizindua Septemba 12 mkoani Mtwara.

Vyama vingine havijaeleza ni lini vitazindua kampeni zao wala maeneo ambayo vitazindulia kampeni ili wananchi waende kusikiliza nini hasa vinatarajia kuyafanya katika kuiletea nchi maendeleo.

Vyama takribani 17 vimejitokeza kushiriki katika uchaguzi huo, ikiwamo kusimamisha wagombea wake wa urais wa Jamhuri ya Muungano na Tanzania Visiwani.

Kwa kutambua umuhimu na uzito wa suala la uchaguzi, tulitarajia kuviona vyama vyote vinavyoshiriki vikiweka wazi mambo yao hususan ratiba zao za kampeni ili Watanzania waweze kufuatilia na kusikiliza ilani za vyama hivyo.

Ilani kielelezo cha nini chama cha siasa kinakusudia kuwafanyia wananchi na ni kwa namna gani kitaweza kufanikisha malengo hayo. Kwa hiyo kila mgombea kuanzia urais, ubunge na udiwani ni lazima anaposimama jukwaani awe ameshika ilani ya chama chake mkononi.

Yale yote anayoyaeleza na kuwaahidi wananchi ni lazima kiwe kimeandikwa kwenye ilani ya chama chake. Kwa lugha nyingine tunaweza kusema kuwa ilani ya uchaguzi ndio mkataba kati ya chama cha siasa na wananchi (wapigakura) baada ya chama hicho kushinda uchaguzi na kushika dola.

Chama chochote kinachoshinda na kukabidhiwa dola, majukumu yake kwa kipindi chote cha miaka mitano hakinabudi kuanza kutekeleza ahadi zake ambazo kiliziainisha katika ilani yake. Kushindwa kufanya hivyo, matokeo yake ni wananchi kukinyima kura katika uchaguzi unaofuata.

Hata hivyo, baadhi ya vyama vinavyoshiriki katika uchaguzi huo vimeshaanza kuonyesha dalili kwamba havitakwenda kufanya kampeni katika mikoa yote nchini kujinadikwa wapigakura.

Wasiwasi huo unatokana na vyama hivyo kutokuonyesha utayari katika maandalizi, hivyo kuviachia vyama kadhaa ambavyo imekuwa ikijitokeza miaka yote ya uchaguzi. Itakumbukwa jinsi uchaguzi wa mwaka 2005, 2025, 2010 na 2015 ulivyojitokeza utitiri wa wagombea wa urais, lakini mwishowe vikashuhudiwa vyama vichache vikifanya kampeni kwa umakini.


Ni jambo lilil0 dhahiri kwamba chama cha siasa kinahitaji rasilimali watu (mtandao wa wanachama) na rasilimali fedha kinapojitosa kushiriki uchaguzi mkuu. Kinyume cha hapo hakuna kinachoweza kufanyika zaidi ya wagombea wake kufanya kampeni za 'kuungaunga' (ubabaishaji).

Hii maana yake ni kwamba wagombea, viongozi, wanachama na wafuasi hawawezi kuwa na uwezo wa kugharamia maadhi ya mambo kama usafiri, chakula, malazi, vifaa vya mikutano ya kampeni na gharama zingine.

Tunavishauri vyama vyote vinavyoshiriki uchaguzi wa mwaka huu kuonyesha umakini kwa kuhakikisha kuwa vinawaendea na kuwafikia Watanzania wote popote walipo nchini kuwaomba kura kwa kunadi ilani zao ili wavione makini, waviamini hivyo wavipe kura, badala ya kuvichukulia kuwa ni vyama vidogo, wababaishaji na wasindikizaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wachunguzeni wanafunzi inakuwaje mlegezo shuleni?

MTINDO wa kubana suruali na kuzivaa kwa kuziegesha , uvaaji uliopewa jina la 'mlegezo' ni miongoni mwa mambo yanayowavutia vijana bila kujali kuwa inawaondolea nidhamu ya mavazi ya shule.

Kulegeza suruali huko kunawateka wanafunzi mbalimbali wakiwamo wa shule za sekondari ambao baadhi 'wanachakachua' sare zao ili kuzipunguza na kuzibana zaidi ili zivaliwe kama 'mlegezo'.

Wapo baadhi ya wanafunzi, ambao hushonewa sare za shule, lakini baadaye huenda kwa mafundi na kuzibadili kwa lengo la kutaka kuvaa mlegezo na kuharibu maana halisi ya sare za shule na kufanya kile wanachotaka.

Wapo baadhi ya wanafunzi wa kiume ukikutana nao katika vyombo vya usafiri au kwenye vituo vya mabasi wamevaa suruali za kubana na wengine wamezishusha kama mlegezo.

Pengine hakuna mwalimu ama mzazi anayeruhusu hali hiyo, bali ni wao wenyewe kwa matakwa yao, wakiamini kuwa ndiyo kwenda na wakati bila kujiuliza huo wakati unawapeleka wapi.

Wadau wa elimu kuanzia wazazi, walezi hadi walimu, wanatakiwa kuliangalia hilo na kuchukua hatua, kwa kuwa haiwezekani kuwaachia wanafunzi kufanya wanavyotaka. Dhana ya nidhamu inatoweka.

Anapoibana, ili iwe anavyotaka, inakuwa siyo sare tena, hivyo wazazi , walezi na walimu wanatakiwa kushirikiana kukomesha hali hiyo ambayo kwa namna moja ama nyingine inaporomosha maadili kwa wanafunzi.

Sare zinatakiwa kufanana kuanzia rangi na mshono, sasa wanapotokea wanafunzi wanazibadili ili ziwe wanavyotaka, wanakuwa wameharibu lengo la sare, hivyo ni vyema wadhibitiwe.

Wakati wanafunzi wa kiume wakibana suruali na kuvaa mlegezo, wenzao wa kike wapo wanaokata sketi ili viwe fupi, kana kwamba wako huru kufanya wanalotaka bila kujali kwamba, ni wanafunzi na sare ndiyo utambulisho wao.

Wanafunzi wa aina ndiyo wale wanaoshinda kwenye vituo vya mabasi wakizurura badala ya kuwahi kwao kupumzika ama kufanya kazi za nyumbani, mara wanaporudi kutoka shule.

Katika vituo mbalimbali vya daladala, jijini Dar es Salaam, wanafunzi wa aina hiyo wa kike na wa kiume wapo, hata kama daladala litakuwa ina nafasi ya kubeba abiria madereva hawawataki.

Kwanza, mwanafunzi mwenyewe ni sehemu muhimu katika kuboresha elimu, ikiwamo utayari wa kujifunza maarifa huku walimu, wazazi na jamii kwa ujumla wakiwa na jukumu la kuwaandaa watoto wao kisaikolojia.

Jambo la kuzingatia katika yote hayo, ni nidhamu kwa mwanafunzi ambayo kimsingi ni moja ya nyenzo za muhimu ya maendeleo na mafanikio shuleni na kwenye jamii.

Wanafunzi kushinda kwenye vituo vya daladala, kubana sare za shule ama kuzikata kuwa fupi ndiyo hao ambao wakati mwingine huwa ni watoro, na kwa hali hiyo, huathiri ufanisi wao shuleni.

Kwa kawaida, wakuu wa shule wanatazamwa kama kiini cha mafanikio ya shule, hivyo wawe wanafutilia wanafunzi wanaobadili sare za shule kuwa katika mitindo wanayotaka na kuwachukulia hatua.

Pamoja na hilo, wawe wanawasiliana na wazazi na walezi kujua ni muda gani wanafunzi hufika nyumbani, kwa kuwa inawezakana wanafika usiku na kusingizia kuwa wanachelewa kutolewa shuleni kumbe hukaa vituoni 'wakipiga porojo.'

Ufuatiliaji ukifanyika kwa ushirikiano, mtindo wa baadhi ya wanafunzi kubadili sare za shule kuwa kama wanavyotaka wenyewe utakwisha, kwa kuwa watakuwa wanatambua umuhimu wa elimu na kuwa na nidhamu.

Mtindo wa baadhi kutoka shule na kwenda kukaa kwenye vituo vya daladala na kupiga stori, nao hautakuwepo, badala yake watawahi kusaidia kazi za nyumbani na kupata muda wa kujisomea usiku.

Kikubwa ni kila mwanafunzi kuwa na nidhamu, kwa kuwa ni moja ya nyenzo muhimu ya kumuwezesha kufanya vizuri katika masomo yake kwa manufaa ya mustakabali wake.

# Ofisa BRELA kortini madai uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

WATU watano akiwamo Msajili Msaidizi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Noel Shani (44), wafanyakazi wawili wa Benki ya Equity na wafanyabiashara wawili, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka ya kughushi na kutakatisha Dola za Marekani 300,000.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa washtakiwa hao wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha fedha.

Wankyo aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni Mohammed Nur (48) raia wa Afrika Kusini, Umulkher Mohammed (34) raia wa Somalia, wote wafanyabiashara.

Washtakiwa wengine ni mfanyakazi wa Benki, Alex Ndondole (33) na mfanyakazi mwingine wa benki hiyo, Emma Chikaonda, ambaye hakuwapo mahakamani.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Machi 2011 na Mei 30, 2016 jijini Dar es Salaam, walikula njama na kujipatia fedha kwa udanganyifu.

Shtaka la pili, mshtakiwa wa kwanza na wapili, wanadaiwa kughushi uamuzi wa bodi ya Kampuni ya Alliance Cargo Handling Ltd ya Februari 8, 2014 kuonyesha kuwa kampuni hiyo imekubaliana kufungua akaunti katika Benki ya Equity tawi la Prestige wakati si kweli.

Shtaka la tatu ni la kughushi ambapo mshtakiwa wa kwanza na pili, Aprili 12, 2015 wanadaiwa kughushi maamuzi ya bodi ya Aprili 12, 2015 wakionyesha kwamba bodi imekubali kufungua akaunti Benki ya Amana tawi la Nyerere Road.

Wankyo alidai shtaka la nne ni kwa mshtakiwa wa kwanza ambaye anadaiwa Aprili 18, 2011 alighushi barua kuonyesha imetolewa na BRELA kwa kuonyesha kwamba Mohammed ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Alliance huku akijua si kweli.

Alidai katika shtaka la tano, mshtakiwa wa kwanza na pili, walighushi uamuzi wa bodi wa Machi 5, 2016 wakionyesha Kampuni ya Alliance inabadili jina kutoka Alliance Cargo kwenda Africa Flight Service Tanzania wakati si kweli.

"Shtaka la sita Februari 8, 2014 mshtakiwa wa kwanza aliwasilisha nyaraka za uongo za uamuzi wa bodi kuonyesha kwamba wamekubali kufungua akaunti Benki ya Equity.

"Katika shtaka la saba mshtakiwa huyo aliwasilisha nyaraka Amana Bank kuonyesha kampuni imekubaliana kufungua akaunti.

"Mshtakiwa anadaiwa kiwasilisha BRELA nyaraka kuonyesha wamekubaliana kubadilisha jina la kampuni," alidai Wankyo.

Alidai katika shtaka la tisa, Februari 10, 2014 maeneo ya Equity Bank, mshtakiwa wa kwanza na pili kwa nia ya kufanya udanganyifu katika akaunti ya Kampuni ya Cargo iliyopo benki ya Equity, walichukua mkopo wa Dola za Marekani 300,000.

Katika shtaka la 10 mshtakiwa wa nne na tano, wanadaiwa kushindwa kuzuia kosa kutendeka, wakiwa maofisa wa benki ya Equity.

Wankyo alidai shtaka la 11, mshtakiwa tatu akiwa Msajili Msaidizi BRELA alishindwa kuzuia uhalifu na shtaka la 12 la kutakatisha linamkabili mshtakiwa wa kwanza na wa pili 2 na shtaka la 13 washtakiwa wote wanadaiwa kutakatisha Dola za Marekani 300,000.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu lolote sababu Mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo la uhujumu uchumi.

Wankyo aliomba washtakiwa warudi polisi kwa sababu hawajapimwa corona. Mahakama ilikubali na walirudi polisi kwa ajili ya vipimo. Kesi itatajwa Septemba 7 mwaka huu.

## RC aagiza kukamatwa mwenyekiti wa kijiji

**Na Tiganya Vincent**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameagiza kukamatwa kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mdaki wilayani Uyui, Charles Wambo, kwa tuhuma za kuchangisha michango kinyume cha taratibu na kuwapatia stakabadhi zinaonyesha fedha walizotoa.

Alitoa agizo hilo jana mjini hapa baada ya mwenyekiti huyo kutuhumiwa kuwa amekuwa akipita kwa kila familia na kuchangisha Sh. 15,000 kwa madai kuwa anazipeleka polisi ili wasiwe wanakwenda usiku kuendesha misako katika kijiji hicho.

Dk. Sengati alisema mhusika ni lazima akamatwe na kufikishwa katika vyombo vya sheria ili kujibu tuhuma zinazomkabili huku akiwataka wananchi kuishi kwa kuzingatia sheria zinazoongoza nchi na kutopenda kutoa fedha kwa nia ya kutaka kuficha maovu.

Pia alisema serikali haina utaratibu kukusanya fedha kwa lengo la kutaka kuzuia misako ya kutafuta wahalifu. Katika hatua nyingine, Dk. Sengati alikabidhi Sh. milioni 185.3 zilizookolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Tabora kutoka kwa wabadhirifu.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tabora, Mussa Chaulo, alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 103.4 zilizorejeshwa ni kutoka kwa wakulima waliouza tumbaku kwenye Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS) cha Imalamakoye, Urambo.

Alisema fedha zingine, Sh. milioni 16.5, ziliokolewa baada ya AMCOS ya Nyota ya Muungano kulipa kama gharama za ujenzi wa ghala, lakini halikujengwa na mkandarasi.

Chaulo alisema Sh. milioni 38.1 ziliokolewa baada ya Mibono AMCOS ya Sikonge kukatwa na Igalula AMCOS kimakosa kupitia mauzo ya tumbaku. Aliongeza kuwa Sh. milioni 25.4 zimeokolewa na kurejeshwa na Chama Kikuu cha Ushirika (WETCU) baada ya kukatwa kimakosa kama gharama za kusambaza mifuko 660 ya mbolea ya NPK.



Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge, akijaribu moja ya magari 14 yakiwamo matrekta matano yaliyonunuliwa na jeshi hilo, kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa miradi mbalimbali katika uzinduzi wa magari hayo, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: ROMANA MALLYA**

# JKT yanunua magari, matrekta ya bil. 2/- kutekeleza miradi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeendelea kujiimarisha kwa kununua magari, matrekta na mashine zenye thamani ya Sh. bilioni 2.383 ili kurahisisha utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Katika mwaka 2020/21, jeshi hilo limejipanga kulima ekari 2500 za mpunga huko Chita, mji wa Ifakara wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa magari na mashine hizo, Mkuu wa jeshi hilo, Meja Jenerali Charles Mbuge, aliishukuru serikali, taasisi na mashirika binafsi kwa kuendelea kuliamini JKT na kulipatia miradi pamoja na kazi mbalimbali.

"Kimsingi azma yangu nikiwa Mkuu wa JKT na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) ni kuhakikisha JKT na shirika linakuwa na magari na mitambo ili kufanya kazi kwa ufanisi," alisema.

Alisema katika kipindi chake cha utawala takriban mwaka mmoja, JKT limenunua magari 26 ambapo upande wa serikali ni matano na wa shirika magari 21.

Kwa upande wa mitambo na mashine, alisema serikali ilinunua mitambo saba na mashine 11 na shirika limenunua mashine sita.

"Tangu niteuliwe kuwa Mkuu wa JKT niliazimia kuliboresha JKT na shirika kwa kuongeza vitendea kazi, na hii leo ninazindua magari 14 ambapo kati yake malori ni tisa na magari ya utawala manne, matrekta matano na mashine 11 yote ni mapya," alisema.

Meja Jenerali Mbuge alisema hivi karibuni jeshi hilo lilizindua magari mengine na pikipiki.

"Ninawataka watendaji wa JKT kwa upande wa serikali na shirika kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi na tija ili kuendana na kasi ya uongozi wa serikali chini ya Rais John Magufuli," alisema.

Alisema kwa kufanya hivyo kutasababisha kuzalisha kwa tija na kupata mapato yatakayosaidia kutekeleza malezi ya vijana na kuliwezesha JKT kutoa gawio kubwa kwa serikali mwaka mpya wa fedha.

Kaimu Mkuu wa Utawala JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema wapo katika mchakato wa ununuzi wa matrekta makubwa ili yaendane na maeneo wanayofanya shughuli za kilimo.

"Huko Chita, Ifakara tupo katika ujenzi wa miundombinu kwa kuanzia tunatengeneza ya hekari 2,500 ambapo kutokana na makandarasi waliopo kule wanasema hadi kufikia mwishoni mwa Oktoba itakuwa imekamilika," alisema.

Alisema kwa msimu mmoja wanatarajia kulima mara mbili kwa mvua na wakati wa kiangazi.

"Katika msimu wa dharura kule Chita tulilima hekari 1,000 za mpunga lakini kwenye mwaka huu wa 2020/21 tumepanga kulima hekari 2,500 za mpunga," alisema.

Kuhusu magari matano waliyokabidhiwa siku hiyo, Kanali Mabena alisema yatasaidia viongozi kutembelea miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa na jeshi hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Brigedia Jenerali, Rajabu Mabele, alisema wamekuwa wakipata miradi mingi ya utekelezaji na changamoto ni vifaa ambavyo Meja Jenerali Mbuge anakabiliana kuitatua.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya SUMAJKT, Meja Jenerali mstaafu Farah Mohammed, alisema ndani ya mwaka mmoja wamenunua vifaa na mitambo mbalimbali.

# Kinana: Msiridhike jitokezeni kupiga kura

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

KATIBU Mkuu mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abrahman Kinana, amewataka wananchi kutoridhika na namna mgombea wa Chama hicho, Dk. John Magufuli anavyokubalika na kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vya kupigia kura siku ya uchaguzi Oktoba 28.

Alikuwa akizungumza jana mjini Miono, Halmashauri ya Chalinze, wakati akizindua kampeni za CCM Wilaya ya Bagamoyo na kuwanadi wagombea ubunge Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete na Bagamoyo, Mwarami Mkenge pamoja na madiwani wa chama hicho.

"Ndugu zangu msiridhike na hali iliyopo huko namna anavyoonekana kukubalika mgombea wetu wa urais, hatari ninayoiona wengi watasema si atapita tu ninachowasihi kupita kwake ni kwenda kumpigia kura," alisema Kinana

Alisema, tegemeo kubwa ni kwa wanachama wa CCM kuhamasisha wananchi siku ya uchaguzi na kwenda kupiga kura ili tufanikishe ushindi wa kishindo kuanzia ngazi ya Rais, Mbunge na Diwani.

"Tegemeo letu wanaCCM, tunawategemea mabalozi, viongozi wa kata na ngazi zote kuhamasisha wananchi kwenda kupiga kura, kampeni ni muhimu, lakini lazima tujipange vizuri kwenda kupiga kura," alisema.

Alisema Rais Magufuli ambaye ni mgombea wa chama hicho ana uwezo mpana wa kuongoza kila jambo, na kwamba wananchi ni mashahidi wazuri kwa kila kilichoahidiwa kimetekelezwa.

Kinana alisema, Dk Magufuli ni kati ya viongozi wenye ujasiri, mwadilifu ambaye ujasiri wake umeonekana katika maamuzi mbalimbali aliyoyafanya katika kipindi chake cha uongozi.

"Tunapata tabu kumsemea kwakuwa wananchi wenyewe ni mashahidi wa yale yaliyofanywa na Serikali ya awamu ya tano, vituo vya afya, elimu, barabara na miundombinu ya maji," alisema.

Kwa upande wake mgombea Ubunge Jimbo la Chalinze Ridhiwani Kikwete, alisema kitu anachojivunia katika kipindi chake cha miaka mitano iliyopita ni wananchi kupata huduma ya maji ambayo ilikuwa changamoto ya muda mrefu kwao.

Ridhiwani alisema, maji ilikuwa kikwazo cha maendeleo katika jimbo hilo na kwamba hadi sasa ni vijiji vichache katika eneo lake ambavyo having maji na katika awamu ijayo vitafikiwa na huduma hiyo.

"Vipo vipaumbele katika awamu ijayo ambayo tutavitekeleza katika jimbo letu, miaka mitano ijayo ni ya kazi kubwa kutekeleza miradi ya maendeleo ya kuwasaidia wananchi ikiwa ni pamoja na kumaliza kazi ya usambazaji wa maji maeneo ambayo hayajafikiwa," alisema Ridhiwani.

Alisema Chalinze haiwezi kupata maendeleo endapo hawatampigia kura Dk. Magufuli kuongoza katika kipindi kingine cha miaka mitano kwa nafasi ya Rais na kuwaomba viongozi wa chama na wanachama kumsemea yale yaliyotekelezwa na Rais wa awamu ya tano kwa wananchi.

Mgombea udiwani kata ya Miono, Juma Mpwimbwi alimuomba Kinana kumfikishia salamu Rais Magufuli kusaidia kuwawekea lami kilomita 21 kutoka Mandela hadi Mkange.



Mwendesha bodaboda akiwa amepakia gunia la mihogo na abiria juu katika eneo la Chanika, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Vijana Wasabato wapewa siri ya fursa za uwekezaji

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Waadventista Wasabato Jimbo la Mashariki Kati, Mchungaji Joseph Mngwabi, amewataka vijana wa kanisa hilo kuepuka uvivu, badala yake kuwekeza kwenye kazi za kilimo ili wajipatie kipato.

Mchungaji Mngwabi yaliyasema hayo juzi kwenye Sikukuu ya Vibanda (Makambi) ya Mtaa wa Nanenane Manispaa ya Morogoro ambapo aliwataka vijana wa kanisa hilo kufanya kazi za mikono kama za shamba ili wajipatie kipato cha kutosha.

"Natumia fursa hii kuwataka vijana wa kanisa hili kuwa mfano wa kuigwa katika jamii juu ya suala zima la kujipatia kipato kutokana na kilimo kwani ili waweze kufanikiwa kimaisha ni wajibu wa kila mtu alime shamba," alisema Mngwabi.

Mchungaji huyo alisema kila mtu hususani vijana anatakiwa kutumia mafundisho ya sikukuu za vibanda mwaka huu kutengeneza njia zao, ambapo alitumia kitabu cha Hosea 10:12 kuelezea namna ya kijana kulima mashamba.

Alisema Kitabu cha Hosea 10:12 maandiko yanaeleza kuwa: "Jipandieni katika haki, vuneni kwa fadhili, uchimbueni udongo wa mashamba yenu kwa maana wakati umewadia wa kumtafuta Bwana hata atakapokuja kuwanyeshea haki."

Mbali na kuwataka vijana kuwekeza kwenye kilimo, pia Mchangaji Mngwabi aliwataka kuwa kioo kizuri kwa jamii ikiwamo kuwa waaminifu ili watu wawezeke kumutukuza Mungu kupitia matendo yao.

Mzee wa kanisa anayesimia kanisa la Kitungwa, Mchungaji Emanuel Kimbawala, aliwataka vijana kujiepusha na tamaa badala yake wamtangulize Mungu kwa kila kitu.

Mchungaji Kimbwawala alisema kuwa baadhi ya vijana wamekuwa wajikijihusisha na tamaa za kimwili na kujikuta wakimkosea Mungu kwa kutenda dhambi, hivyo aliwataka wawe waaminifu katika maisha ya ujana wao.

# Waajiri watakiwa kuweka usalama, afya ya wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAAJIRI mkoani Kilimanjaro wametakiwa kuwekeza kwenye masuala ya usalama na afya kwa wafanyakazi.

Kauli hiyo ameizungumza jana kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, kwenye uzinduzi wa mkakati wa kupunguza ajali na magonjwa sehemu za kazi, maarufu kama Vision Zero Mjini Moshi.

Kundya, alisema endapo waajiri watawekeza kwenye masuala ya usalama na afya mahala pa kazi, kwa kuweka mikakati endelevu ya kuwalinda wafanyakazi, wataweza kuongeza tija kwenye uzalishaji kwenye maeneo ya kazi sambamba na kuongezeka kwa mapato pamoja na ulipaji kodi hivyo kuchangia kukuza uchumi wa taifa.

Akizungumza kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa OSHA, Mkurugenzi wa Usalama na Afya, Mhandisi Alex Ngata, alisema, mafunzo hayo yameandaliwa mahususi kwa ajili ya kuwawezesha waajiri nchini, kuhakikisha wanapunguza ama kuondoa kabisa ajali na magonjwa sehemu za kazi.

Mhandisi Ngata alisema mafunzo hayo ambayo tayari yamefanyika katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na sasa Kilimanjaro, yatawasaidia waajiri kuweka mikakati madhubuti kwenye maeneo yao kazi.

''Sambamba na mafunzo hayo, vile vile tunapata wasaha wa kusikiliza kero na changamoto zao, wakati wa utekelezaji wa sheria na 5 ya mwaka 2003 ya Usalama na Afya, na kuzitatua," alisema Ngata.

Ofisa Mtendaji wa Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Nchini (TCCIA)Mkoa wa Kilimanjaro, Boniface Mariki, alisema mafunzo hayo yatawasaidia katika utendaji kazi wao, kwani wafanyakazi ni kiungo katika utekelezaji wa shughuli za viwandani, endapo mfanyakazi ataumia, itakuwa gharama kubwa kiuchumi, kwanza kumtibia na vile vile, shughuli za uzalishaji zitaathirika.

Alisema wanachama wake wamefurahi kupata mafunzo hayo kwani Vision Zero ni mpya kwao, na hivyo wameahidi kutekeleza ipasavyo mkakati huo ambao umelenga kupunguza ajali na magonjwa sehemu za kazi, na kuiomba OSHA kuendelea kuwapatia mafunzo kama hayo.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Tathimini kutoka Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi (WCF), Dk. Abdulsalum Omari, alisema waajiri wanapaswa kufanya tathmini ya hali hatarishi sehemu zao kazi kwa kutengeneza shabaha ili kutambua kuna ajali kiasi gani na magonjwa kiasi gani, ili waweze kuweka mifumo ya kudhibiti ajali na magonjwa sehemu za kazi.

Mkuu wa Kitengo cha Sheria kutoka OSHA, Joyce Mwambungu, alisema katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, wakala umelenga kujenga uelewa zaidi kwa wadau wake masuala mbalimbali ya usalama na afya, ili kututua changamoto wakati wa utekelezaji wa sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

"Tozo za mafunzo zipo kisheria zinabaki kama ilivyo, ila tozo ya Elimu kwa Umma ndio imefutwa, hivyo waajiri watapatiwa elimu hiyo bure ambayo ilikuwa ikitozwa endapo OSHA itakuja kukupatia elimu," aliongeza Mwambungu.

# Waganga tiba mbadala 122 wasajiliwa Tunduru

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

IMEELEZWA kuwa jumla ya waganga na wataalamu wa tiba mbadala 122 wamesajiliwa na kupatiwa vibali vya Serikali kwa ajili ya kutoa huduma ya tiba kwa wakazi wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma na maeneo mengine.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, idadi hiyo ni kati ya wataalamu wa kutoa huduma hiyo 228 ambao walitambuliwa kuwa wamekuwa wakitoa huduma ya tiba asili na tiba mbadala wilayani humo.

Mbali na waganga hao, pia lipo kundi jingine la waganga 106 ambao wamejiorodhesha kwa ajili ya kuomba vibali kwa ajili ya kutoa huduma hiyo ukiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali linalowataka waganga wote wa tiba asili na tiba mbadala kusajiliwa na kupata vibali badala ya kufanya shughuli zao bila kufuata sheria.

Hayo yalielezwa na Mratibu wa kifua kikuu na ukoma wa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru, Dk. Mkasange Kihongole, kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungumza na wataalamu hao alipotembelea baadhi ya vilinge vya waganga wa tiba asili na tiba mbadala katika vijiji vya Ligoma ,Kadewele na maeneo ya Tunduru mjini kwa lengo la kukagua utendaji wa kazi kwa waganga waliopata vibali vya serikali.

Vibali hivyo vinawezesha utoaji wa tiba hizo kwa wananchi.

Alisema Serikali kupitia kitengo cha tiba asili na tiba mbadala inaendelea kuwasaka baadhi ya waganga wasiosajiliwa ili nao waweze kupata vibali na kutoa huduma hiyo kwa jamii kwa uhakika.

Aidha, kupitia taarifa hiyo, aliwataka waganga wa tiba asilia ambao hawajasajiliwa kujitokeza haraka na kutimiza masharti hayo kabla hawajakamatwa kupitia msako unaotarajiwa kufanyika wakati wowote kuanzi sasa.

Alisema Serikali inataka waganga wote wasajiliwe kwa lengo la kuwatambua na kufahamu shughuli zao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti waganga wa tiba asili na tiba mbadala Shaibu Mkuli wa Kijiji cha Ligoma na Wadin Ngaharo wa Jikiki cha Kadewele, waliipongeza Serikali kwa kuthamini kazi kubwa inayofanywa na waganga hao kwani sasa wanafanya shughuli zao kwa uwazi tofauti na awali ambapo baadhi ya watu waliwaona kama matapeli.

Walisema baada ya Serikali kuwapatia mafunzo ya namna ya kuwaibua wagonjwa wa kifua kikuu, kumekuwa na mafanikio makubwa kwani kwa muda mfupi wameweza kuwabaini watu wenye vimelea vya ugonjwa huo na kuwapa rufani ya kwenda hospitali ambako baada ya vipimo wamebainika kuwa na maradhi hayo.

**Serikali kupitia kitengo cha tiba asili na tiba mbadala inaendelea kuwasaka baadhi ya waganga wasiosajiliwa ili nao waweze kupata vibali na kutoa huduma hiyo kwa jamii kwa uhakika.**

# Madaktari China wapiga jeki vifaa vya mil. 200/-

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

VIFAA tiba, dawa na vitabu vya mwongozo wa matibabu vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni 200 vimetolewa na madaktari kutoka China ambao wanafanya kazi katika hospitali ya Addalla Mzee Mkoa wa Kusini Pemba.

**upatikanaji wa vifaa hivyo utapunguza changamoto na kuhakikisha wanavisimamia ipasavyo, ili vitumike kwa muda mrefu.**

Kiongozi wa timu ya 29 ya madaktari kutoka China, Dk: Youan Tongzhou, alisema, utoaji wa vifaa tiba hivyo na dawa ni kutokana na uzalendo walionao kwa ushirikiano mazuri kati ya wafanyakazi, uongozi wa hospitali na Wizara.

Alisema kutokana na wagonjwa wanaofika katika hospitali hiyo, wameona kwamba kuna matatizo mengi ambayo huwatokezea wananchi, ambapo hushindwa kuyamudu kimatibabu na ndio maana wakaamua kusaidia vifaa hivyo ili kupunguza changamoto.

Akizungumza wakati akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Wilaya Mkoani, Dk: Youan, alisema, wameamua kutoa msaada huo kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa kisiwa cha Pemba na wale wanaotoka nje ya Pemba.

"Tangu tuanze kufanyakazi Hospital Abdalla Mzee ni mwaka sasa, tumeona mambo mengi ambayo yanahitaji kusaidiwa ikiwamo vifaa tiba, hivyo tumejitolea binafsi kwa mapenzi makubwa ya wananchi wa Pemba," alisema Dk: Yuan.

Akipokea vifaa hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Issa Juma Ali, alisema, uwapo wa madaktari hao wanajivunia sana kwa kupata misaada mbalimbali katika hospitali hiyo na kusema hiyo ni kutokana na ushirikiano ya viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais-Dk: Ali Mohamed Shein kwa kuwajali wananchi wake katika kuwafikishia huduma za kijamii.

Mkuu huyo alimshukuru kiongozi wa timu hiyo kwa kujitolea kwa moyo wa dhati kusaidia na kuwataka wafanyakazi kuwa wazalendo na kuzidisha ushirikiano kwao ili kupata misaada zaidi.

Aliwataka wafanyakazi hao kuvitunza, kuvithamini na kuvilinda vifaa hivyo ili vidumu kwa muda mrefu, jambo ambalo litasaidia kutatua changamoto zilizopo kwenye hospitali hiyo na kusema kuwa hawatamvumilia daktari yeyote atakaetumia vifaa hivyo kunyume cha makusudio.

Akitoa shukrani kwa msaada huo, Ofisa Uendeshaji Tiba kutoka Wizara ya Afya Pemba, Dk: Yusuf Hamadi Iddi, aliipongeza timu ya 29 ya madaktari kutoka China kwa kuwapatia msaada huo muhimu na kuwa vitawasaidia sana hasa kwa wagonjwa wa ajali.

Mganga Mkuu wa Hospital ya Abdallah Mzee, Haji Mwita Haji, alisema upatikanaji wa vifaa hivyo utapunguza changamoto na kuhakikisha wanavisimamia ipasavyo, ili vitumike kwa muda mrefu.

Nao wafanyakazi wa hospitali hiyo walisema vifaa vilivyotolewa ni muhimu na kuwa watavitumia kama ilivyokusudiwa.



Wakazi wa kijiji cha Msufini, Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, wakishiriki katika kazi ya kusomba udongo kujaza kwenye vyumba vipya vya madarasa wanavyovijenga kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Msufini, juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mtwara yapaisha miradi uwekezaji

**Na Mwandishi wetu,** MTWARA

MKOA wa Mtwara unaendelea kuimarisha miundombinu inayochangia kukua kwa uwekezaji ukiwamo upanuzi wa Bandari ya Mkoa huo uliogharimu Sh. bilioni 157.

Uwekezaji mwingine ni ujenzi wa njia nyingine ya kurukia ndege unaogharimu Sh. bilioni 50.

Katibu Tawala wa mkoa huo, Alphayo Kidata, ndiye aliyebainisha hayo na kusema lengo la ujenzi wa miundombinu hiyo ni kuhakikisha mkoa huo unafungua njia zake za kiuchumi hususan kwenye kilimo cha korosho na uwapo wa gesi asilia ambayo imekuwa chachu ya uanzishwaji wa viwanda ambavyo vimekuwa na tija ya kiuchumi.

Kidata aliyasema hayo wakati akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, alipotembelea Mkoa huo ikiwa ni sehemu ya ziara yake katika Kanda ya Kusini yenye lengo la kuangalia fursa na changamoto za uwekezaji.

"Mtwara tumejipanga kupokea uwekezaji, tunao wawekezaji wanaofanya vizuri na tunazidi kukaribisha wengine wengi, tunazo fursa na miundombinu yote, pia kwa sasa tunaendelea kuimarisha ujenzi wa miundombinu mingine ya kisasa ya usafirishaji ikiwamo Bandari na uwanja wetu wa ndege, kwa hiyo msiwe na wasiwasi," alisema Kidata

Dk. Kazi pamoja na kuipongeza Serikali mkoani humo kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo ambayo inasaidia kurahisisha uwekezaji, alitoa wito kuendelea kuhamasisha uwekezaji pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli hiyo.

"Naomba tu niwapongeze, kazi ya kuvutia uwekezaji mnayoifanya ni njema, sisi tunawaunga mkono na pia msisite kuileta TIC pale zinapoonekana changamoto," alisema Dk. Kazi.

Mkuu wa Wilaya Mtwara, Dunstan Kyobya, alisema milango ya uwekezaji katika sekta zote ipo wazi katika wilaya yake ambayo imekuwa ikipokea wageni wengi kuliko maeneo mengine ya mikoa ya Kanda ya Kusini.

# Mfumo wa kidigitali kupaisha ufaulu Moro

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKOA wa Morogoro umejipanga kuongeza ufaulu katika shule za msingi na sekondari mijini na vijijini na kuwawezesha wanafunzi kufanya mawasiliano mazuri na nchi nyingine kupitia mfumo wa kidigitali unaojulikana kama Teschools.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Joyce Baravuga, wakati wa uzinduzi wa mfumo huo.

Alisema kuwa mfumo huo utawasaidia wanafunzi kuongeza ufaulu kwa kujifunza mambo mengi kutoka kwa wanafunzi wengine nje ya nchi na kupata taarifa kwa haraka.

"Tumeamua kufanya mchakato huu na kwa sasa Mkoa wa Morogoro tulikuwa tumedhamiria mfumo huu wa kidigital utaanza kutunika mwaka 2020, lakini tunaona mfumo huu umekuja kwa kasi na lengo letu ni kufikia shule zote za sekondari na msingi zilizopo katika Manispaa ya Morogoro," alisema Mhandisi Baravuga.

**Tunapenda kuwasaidia wanafunzi hasa watoto wa kike kutambua teknolojia kwani hata mimi nimejifunza mambo mengi kutokana na kufahamu teknolojia.**

Aidha, Mhandisi Baravuga aliwataka walimu na wanafunzi waliopatiwa mafunzo hayo watumie elimu ili iweze kuwasaidia katika kuleta maendeleo katika jamii na kuwaomba wawezeshaji kutoka taasisi za APSS AND GIRLS pamoja na NLAB kutengeneza mfumo huo kwa Tanzania nzima kwa kuwasaidia wanafunzi.

Alisisitiza kuwa sekta ya elimu itasonga mbele kwa kasi kutokana na mfumo huo kuwafundisha wanafunzi wengi kwa wakati mmoja na kuwaahidi kuwa atasimamia vyema, na kuwataka walimu kusimamia kikamilifu suala la TEHAMA.

Carolyne Ekyarisiima, Mkurugenzi wa Taasisi ya APSS AND GIRLS, alisema lengo la kuendesha mafunzo hayo ni kuwasaidia wanafunzi kutambua teknolojia itakayowasaidia katika masomo yao.

Aliongeza kuwa kutokana na ukuaji wa teknolojia duniani, mambo mengi yanaongozwa kwa mfumo wa kiteknolojia na kuwawezesha wanafunzi kufahamiana na wanafunzi wenzao katika mataifa mengine.

"Tunapenda kuwasaidia wanafunzi hasa watoto wa kike kutambua teknolojia kwani hata mimi nimejifunza mambo mengi kutokana na kufahamu teknolojia," alisema Carolyne.

Baadhi ya walimu na wanafunzi waliopatiwa mafunzo hayo waliwashukuru wawezeshaji na kueleza kuwa mafunzo hayo yatawanufaisha kupata elimu ambayo itawasaidia kufungua website, kutengeneza uhusiano mzuri na wanafunzi wengine na kusoma vitabu mbalimbali kwa njia ya mtandao.



Mke wa Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa, Mama Anna Mkapa (kulia), akipokea nishani yenye ujumbe wa maneno ya Rais Mkapa kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Biashara ya DCB, kutoka kwa mjumbe wa bodi ya benki hiyo, Zawadia Nanyaro, walipokwenda kumpa mkono wa pole nyumbani kwake, Masaki, jijini Dar es Salaam, wikiendi. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Godfrey Ndalahwa (wapili kushoto) na Mkuu wa Masoko na Mawasiliano, Rahma Ngassa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sekta binafsi, umma zilivyoshirikiana wakati wa corona

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imesema ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona ulipokuwa umeshika kasi duniani, sekta binafsi ilishirikiana na sekta ya umma kutengeneza mkakati wa uendeshaji wa shughuli na biashara ya utalii.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Arusha na Katibu Mkuu Wizara ya Malisiali na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika warsha ya kupokea maoni ya wadau wa utalii katika kuandaa mkakati wa kurejesha sekta ya utalii katika hali yake ya awali baada ya kupungua kwa mapambano dhidi ya COVID-19.

''Tulitengeneza mkakati huo ambao unaitwa Standard Operate Procedures ili kuhakikisha kwamba tunaishi na ugonjwa huu kwa maana ya kwamba tusisimamishe shughuli za kuwapokea watalii, lakini tujue namna ya kuwapokea watalii ili kusudi wawe salama na watoa huduma wawe salama," alisema.

Katika mkakati huo, alisema waliahidi kwamba katika maeneo yao ya utalii wataweka magari ya kubebea wagonjwa pamoja na kuandaa maeneo ambayo yatasaidia kutoa huduma pale, ambapo ikitokea watalii wamepata tatizo ama watoa huduma wamepata tatizo waweze kuhudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Wakati huo huo, amelishukuru Shirika la Kimataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) kwa kushiriki kuandaa na kuboresha magari ya kubebea wagonjwa kwa kuyabadilisha magari hayo kutoka ya kawaida na kuwa magari ya kubebea wagonjwa, ambayo yatasaidia kuhudumia watalii watakaopata dharura za maradhi pindi wakiwa katika ziara zao.

"Tunalishukuru Shirika la UNDP limefadhili pamoja na kugharamia magari hayo. Tunashukuru sana kwa kutusaidia na sasa wanatusaidia kazi nyingine maarufu na muhimu sana ambayo ni ya kutengeneza mkakati wa kurejesha hali ya utalii kama ilivyo kuwa awali."

# Dawa ya udumavu kwa watoto yatajwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANAWAKE wameshauriwa kutumia vyakula vinavyoongeza damu ili kuepukana na vifo vinavyotokana na uzazi.

Sababu nyingine ni kuepukana na watoto wanaozaliwa kuwa na udumavu, ambao wanakuwa na uelewa mdogo wakati wa kujifunza.

Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Prisca Nyambo, alitoa ushauri huo juzi alipokuwa akifundisha wajawazito, kinamama na wanaume wanaokwenda kliniki kwenye Kituo cha Afya cha Mwendapole.

Nyambo alisema ili mama mjamzito ajifungue salama, lazima kuwe na maandalizi kabla ya kupata ujauzito kwa kula vyakula ambavyo vitamfanya awe na damu ya kutosha wakati anamimba hadi anapojifungua.

Alisema, upungufu wa damu husababishwa na kutokwa damu nyingi tatizo ambalo limekuwa likikua siku hadi siku nchini, na kwamba huanzia kwenye mimba.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Tulitweni Mwinuka, alisema katika kutoa huduma za afya ya uzazi, wamegundua baadhi ya changamoto ni upungufu wa damu kwa wajawazito na watoto kuwa na udumavu.

Alisema, kutokana na hali hiyo, walianzisha kampeni kuwafundisha wanawake kwa vitendo kwenye kliniki ya uzazi na mtoto (RCH) pamoja na kuhamasisha uandaaji wa vyakula.

Dk. Mwinuka alisema wamepanga kuvifikia vituo vyote 12 vinavyotoa huduma ya uzazi na mtoto na vya binafsi, lengo ni kutokomeza vifo vya kinamama na watoto.

Ofisa mradi wa Taasisi ya Shirika la Msaada la Serikali ya Watu wa Korea (KOFI) linalosaidia kwenye sekta ya afya kudumisha afya ya mama na mtoto mkoa wa Pwani, Dk. Nyasatu Mwendwa, alisema mjamzito hapaswi kupoteza maisha wakati akijifungua kwa kukosa damu.

Dk. Nyasatu alisema wanapambana kuhakikisha vifo havitokei kwa wanawake wakati wa kujifungua, na kwamba wamebaini ukosefu wa elimu kwani hawajui umuhimu wa damu ni wajibu wahakikishe kipindi cha mimba kinaisha bila kuongezewa damu ili kuwalinda wao na watoto.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 1, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**UN: COVID 19 Imevuruga utalii, kuharibu ajira, uchumi, urithi wa asili**



Ukurasa 13

KITISHO MOTO
Kilimo, radi, kiangazi vyatajwa kuleta balaa



Ukurasa 12

**Biashara mtandaoni Kinamama watoboa kipindi cha corona**

SAYANSI
**NA AGNES TEMU**

## RUFIJI NI MAAJABU
# Umeficha mji uliozama, wataalamu kuujenga upya

ULE usemi kuwa ukistaajabu ya Musa utayaona ya Farao, unaweza kuhusishwa na taarifa zinazoelezwa na Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kuwa kinajiandaa kuufukua na kuujenga upya mji wa kale uliozama ndani ya delta ya Mto Rufiji mkoani.

Mji huo uko pale mto huo unapomwaga maji ndani ya Bahari ya Hindi, kinasema Kitengo cha Utafiti wa Binadamu na Mambo ya Kale cha UDSM.


Kinachofanya sasa ni kuanda utafiti wa kupata taarifa za mji wa kale uliozama ndani ya maji kwa nia ya kuujenga upya na kuufanya kuwa miongoni mwa vivutio na kitovu cha utalii duniani anasema, Profesa Felix Chami.

Mji huo uliojulikana kama Rhapta,ulikuwepo miaka 2,000 kabla ya Masiha Yesu Kristo na kwamba ulijengwa katika delta mto Rufiji na ulizama ndani ya Bahari ya Hindi kutokana na sababu ambazo hazijafahamika.

Anaeleza Mkuu wa Kitengo Cha Utafiti wa Binadamu na Mambo ya Kale, wakati wa mahojiano na Nipashe, jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Mwanazuoni huyo wa historia na akiolojia anasemaa ili kufikia azma hiyo wanaandaa bajeti katika vitengo tofauti ili kujua gharama, taratibu za kazi hiyo na namna ya kuikamilisha ili kutafuta pesa za utafiti.

Anafafanua: "Baada ya kuhitimu shahada ya uzamivu niliamua kufanya utafiti mwaka 1995, katika mijini ya pwani ikiwamo Bagamoyo, Zanzibar, Tanga na Rufiji na kugundua kulikuwapo na mji huo."



Mabaki ya ukuta wa Raphta uliokuwa chini ya maji ni wa mraba kuashiria kuwa ni kazi ya binadamu. **PICHA: PROFESA FELIX CHAMI.**

Profesa Chami anasema kuwa utafiti wake ulilenga kujua binadamu wa kwanza aliyeishi pwani alikuwa ni nani mzawa au mgeni kutoka mataifa ya Uajemi (Mwarabu)? Utafiti umeonyesha kuwa Mwafrika ndiyo wa kwanza kuishi pwani ya Tanzania na mji huu mwanzo ulijulikana kama 'Zaa' wenyeji wakiuita 'Zaania' wakimaanisha 'maji mengi'.

Mtafiti huyu anaeleza kuwa kutokana na utafiti wake aligundua kuwapo kwa kitu cha tofauti katika Bahari ya Hindi kandokando ya kijiji cha Jojo baada ya kuona udongo wenye weusi usio wa kawaida, lakini kutokana na kukosa vifaa vya kupima atahitaji kuchunguza zaidi.

"Wakati nafanya utafiti sikuwa na vifaa vyenye uwezo hivyo niliposwauliza wenyeji pale kuna nini walisema ni mchanga unajaa sana ukienda unazama hutoki. Nikaogopa nikaondoka.

"Mwaka 2016 alipita Mzungu na helikopta aliona weusi usio wa kawaida akashuka akapima na vifaa vyake akagundua kuwapo kwa mawe makubwa baada ya kusoma utafiti wangu alinitafuta, kwa pamoja tukagundua kuwa kuna mji uliozama miaka 2,000 iliyopita kabla ya kuzaliwa Kristo."

Anaongeza kuwa kutokana na kukosekana kwa fedha za kufanya utafiti ilibidi kuomba pesa za utafiti kwa mmiliki wa hoteli ya Shungimbili kisiwani Mafia kwa ahadi kuwa wakifanikiwa atanufaika .

Hata hivyo, utafiti haujakamilika licha ya msaada wake na mwaka huu serikali imeagiza kuandaliwa bajeti kuuendeleza utafiti uliokwama kutokana na kukosekana pesa.

### KINACHOJIRI MAJINI

Profesa Chami anaeleza kuwa Rhapta au Zaania ni mji uliozama ukiwa na urefu wa kilometa nne, upana wa kilometa tatu ndani ya maji kwenye eneo mto Rufiji unapoingia kwenye Bahari ya Hindi na kwamba kuna picha za mabaki ya vyumba ndani kukiwa na chupa za manukato.

Anasema Waarabu walipofika walibadili jina la Zaa na kuita Rhapta ambapo ndiyo ilikuwa ni makao makuu yao na kwamba Zaa hadi Zanzibar ni kilomita 30 au safari ya siku moja kwa mashua.

Anaeleza kuwa utafiti huu utalihamasisha Shirika la Elimu , Sayansi na Utamaduni (UNESCO) chombo cha dunia kuunga mkono na kuchochea watalii kuzuru Tanzania kuuona mji uliozama. Wakati Profesa Chami, akihojiwa hivi karibuni na vyombo vya habari alitaja serikali kutokuweka bajeti endelevu ya utafiti kama ilivyo katika utafiti wa masuala ya magonjwa ndiyo changamoto iliyokwamisha jitihada hizo.

"Kama ingekuwepo bajeti ya kutosha ningeibuka Mtanzania wa kwanza kugundua mjini uliozama. Lakini kwa kukosa vifaa, mgeni amekuja navyo baada ya kusoma utafiti wangu ndiyo akaufanyia kazi,"anasema kwa uchungu.

### MIJI MINGINE ILIYOZAMA

Iwapo utafiti huo utafanikiwa Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi saba duniani ambazo miji yao ilipozama walitengeneza fursa za uwekezaji kwa kuijenga na kuifanya vivutio vya utalii duniani.

Miji hiyo ni Dwarka uliopo India wenye futi 70,chini ya bahari jirani na kisiwa cha Bet Dwarka katika jimbo la Gujarat. Inakadiriwa kuwa ulijengwa kati ya miaka 9,000 hadi 12,000, iliyopita kabla ya Kristo. Unapoutembelea una majengo ya thamani ikiwa ni pamoja na barabara,bandari na kuta zilizojengwa kwa mchanga wa bahari.

China kuna mji wa kale wa Lion City -Mji wa Simba uliofichwa chini ya Ziwa Giandao ambapo hapo awali ulijulikana kama Shichang na huko kunaelezwa kuwa ndicho kilichokuwa kitovu cha siasa na uchumi kwenye jimbo la Mashariki ya Zhang.

Wataalamu wa mambo ya kale wanaeueleza kuwa ni jiji lililopo futi 130 chini ya maji na ndani yake kuna majengo ya kale yaliyojengwa miaka 10,000 yenye mahekalu na michoro ya kutisha ya nyoka wa ajabu.

TEKINOLOJIA

NA JENIFER GILLA

# Biashara mtandaoni Kinamama watoboa kipindi cha corona

“SIKUPATA wasiwasi na mwenendo wa biashara yangu kwa sababu naifanya tofauti”.

Ni maneno ya Bertha Mmari ( 33) Mkazi wa jijini Dar es Salaam, akiwa na uso uliojaa furaha na sauti ya kujiamini, alipokuwa akizunguzia mwenendo wa biashara yake katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19, unaosababishwa na virusi vya corona kwa mwandishi wa gazeti hili.

Bertha ni mmoja kati ya wafanyabiashara wanawake wachache nchini, wanaojivunia uwapo wa mitandao ya kijamii, kwani imekuwa mkombozi wa biashara zao hivyo kupata mafanikio makubwa tofauti na wafanyabiashara wengine.

Licha ya mama huyu kumiliki duka la nguo za kike, viatu na pochi Kariakoo, asilimia 50 ya wateja wake huwapata kupitia ambao wegi wako ni ‘mawinga’ ambao nao hununua na kuuza kwa njia ya mtandao pia.

“Nilianza na biashara na mtaji wa Shilingi 2,000,000 mwaka 2015 sasa unakaribia milioni 25, wateja wa mitandaoni ndiyo wamenifikisha hapa kwa kiasi kikubwa” anasema Bertha. Tofauti na wafanyabiashara wengine ambao wameathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na shughuli kukosa wateja katika kipindi cha likizo ya ugonjwa wa Covid-19, hadi kupelekea kufunga biashara zao kwa muda, kwa upande wake haikuwa hivyo .

Siri ya kutoyumba kwa biashara yake ni mazoea ya wateja wake kuchagua bidhaa kutoka kwenye akaunti zake za biashara na kulipia kisha anawapelekea walipo.

Akielezea jinsi alivyoingia kwenye biashara ya mtandaoni anasema mwaka 2016, alipiga picha akiwa mevaa gauni analoliuza na kuweka kwenye ukurasa wake wa facebook na kuandika kuwa analiuza, alistaajabu kupata muitikio mkubwa kutoka kwa marafiki zake hao wa mtandaoni.

“Siku niliyoweka nguo kwenye ukurasa wangu, nipata ‘likes’ 200 na maombi 10, hapo ndipo nilipoona umuhimu wa mitandao, ndipo nikafungua ukurasa maalumu kwa ajili ya kuuza bidhaa wa facebook na Instagram,” anaelezea.

Kwa mujibu wa mfanyabiashara huyo, katika kipindi hiki cha mlipuko wa Covid-19 wateja wa mtandaoni wameongezeka mara mbili zaidi na kumuongezea mauzo.

Kwa sasa anapokea maombi ya wateja 15 hadi 20 kwa siku, mara mbili zaidi ikilinganishwa na kabla ya ugonjwa wa corona na kumfanya kuuza bidhaa za Sh.300,000 hadi 500,000 kwa siku.

Bertha si peke yake anayefaidi matunda ya matumizi mazuri ya mtandao. Tuma Ifran pia ni mmoja wa wanawake ambao biashara zao zimeendelea vizuri kipindi cha mlipuko wa virusi vya corona.



Ashura Selemani, mmoja wa wafanyabiashara mtandaoni , akiandaa mzigo wa vyombo alivyonunua mteja.

Mfanyabiashara huyu wa vyombo katika eneo la Mlandege, Zanzibar anasema hajapoteza wateja katika kipindi cha corona tofauti na wafanyabiashara wenzie katika eneo hilo.

Kwa siku hupokea maombi ya wateja 10 hadi 15 kutoka Bara na Zanzibar hivyo kujipatia kati ya Sh.100, 000 hadi 300,000 kwa siku.

Tuma anashukuru kuwapo kwa mtandao wa kijamii kwani kumemfanya kujulikana kila kona ya Tanzania huku akitaja uaminifu kuwa nguzo muhimu ya biashara yake.

Kuongezeka kwa idadi ya wanawake wanaofanya biashara kupitia mitandao ya kijamii kunaelezwa kuwa kutokana na uhamasishaji unaofanywa na wanawake wengine.

Karen Alfred, ni mkurugenzi wa mashamba ya AKSVIN yaliyoko Bagamoyo yanayozalisha mazao mbalimbali, amekuwa akiwashawishi wakulima wanawake kutumia fursa ya mitandao ya kijamii kuuza mazao yao.

Kwa kupitia program ya Uthubutu wa Mwanamke anaiyoiendesha, Karen pamoja na wanawake wengine waliopata mafanikio kupitia mitandao ya kijamii wanaandaa mikutano ya kuwakutanisha wanawake mara kwa mara na kuwaelimisha kuhusu fursa hii.

“Mpaka sasa mradi wetu umewafikia wanawake takribani 300 na tunawafuatilia kwa ukaribu kuona maendeleo yao na kuwapa mbinu za kujiongezea, anasema Kareen ambaye amekuwa akitumia mtandao ya kijamii kwa miaka saba sasa.

> “Katika semina zetu tunawahamasisha wanawake kutumia mitandao ya kijamii vizuri na njia za kujilinda mitandaoni, tunafarijika tunapoona kasi ya wanawake wanaotumia mtandao kujiongezea kipato.

Karen anasema amepata mafanikio makubwa kupitia biashara ya mtandaoni lakini kubwa ni kuepuka madalali ambao hunyonya wakulima kwa kununua mazao kwa bei ya chini na kuyauza kwa gharama kubwa ili kupata faida kubwa. Hivyo, anashauri wanawake kutumia mitandao ya kijamii kujiongezea kipato na sio kufanya sehemu ya maisha ambayo kwa kiasi kikubwa sio halisi kwao.

Meneja wa Zaina Foundation, inayofundisha wanawake kuhusu haki na usalama katika matumizi ya mitandao ya kijamii (digital security), Zaituni Njovu, anaeleza kufarijika kuona wanawake wakitumia mitandao hiyo kwa malengo chanya.

“Katika semina zetu tunawahamasisha wanawake kutumia mitandao ya kijamii vizuri na njia za kujilinda mitandaoni, tunafarijika tunapoona kasi ya wanawake wanaotumia mtandao kujiongezea kipato.

“Hii ina maana kwamba elimu imewafikia na wanaitumia vizuri haki yao ya kutumia mtandao, hivyo tunapata nguvu ya kuendelea kuhamasisha” anaeleza Zaituni.

Kwa mujibu wa Ibrahim Salim, Mkurugenzi wa Mradi na Mawasiliano kutoka asasi ya Action for Rural Women Empowerment(ARWE), kuna idadi kubwa ya wanawake wanaotumia mitandao ya kijamii lakini ni wachache inayowanufaisha.

Hivyo, anashauri serikali pamoja na asasi binafsi kuendelea kutoa elimu kwa wanawake kuhusu fursa zinazopatikana katika mitandao. elimu inatakiwa iendelee kutolewa

CHANGAMOTO

Kukosa simu janja (smartphone) kunaelezwa kuwa ni changamoto inayowazuia wanawake wafanyabiashara kutumia mitandao kujitangaza.

Mwanaija Hamisi, mfanyabiashara wa pochi za mtumba katika soko la Mwenge jijini Dar es Salaam, anayetamani kufanya biashara mtandaoni lakini hana uwezo wa kununua simu janja.

“Simu nzuri kwa sasa ni kuanzia Sh. 100,000 na kuendelea, sasa mimi uwezo huo sina, nikipata mtu wa kuniwezesha nitafanya biashara ya mtandao.” Anasema Mwaija.

Tangu kuingia virusi vya corona mauzo ya Mwaija yalishuka kutoka Sh.70, 000 hadi Sh.20,000 kwa wiki hali inayofanya biashara yake kudhoofika kadiri siku zinavyokwenda .

Kwa sasa watumiaji wa mtandao duniani wamefikia 4.5 bilioni kati ya hao Watanzania ni milioni 23, kwa mujibu wa taarifa za mitandao ya simu ya kimataifa.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka mtandao wa Economic Intelligence Unit, wanawake ndio wanaongoza kutumia mtandao kwa asilimia 52 tofauti na wanaume ambao ni asilimia 21.

Hata hivyo, ripoti ya mtandao wa maarufu wa matumizi ya simu wa GMSA kwa mwaka 2019, inasema kuwa gharama kubwa za simu zinawazuia wanawake kutumia mitandao ya kijamii.

Fursa ya matumizi ya teknolojia kwa mwanamke inazungumziwa katika Mpango wa Maendeleo Endelevu namba tano (SDG), ambao unaelekeza kuwa nchi ziwezeshe matumizi ya teknolojia kwa mawasiliano yatumike kama njia mojawapo ya kumuwezesha na kumwinua mwanamke. Sioni linki

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Gueterres, akizungumzia athari za ugonjwa wa COVID-19 katika moja ya mikutano yake, aliagiza serikali za nchi kuweka kipaumbele kwa wanawake na wasichana katika kupambana na ugonjwa huo .

Ni ukweli usiopingika kuwa wanawake na watoto ndiyo wanaoathirika zaidi na ugonjwa wa virusi vya corona.

***Ripoti hii imetayarishwa kwa kushirikiana na Mradi wa Wanahabari Wanawake Afrika na Kituo Cha Kimataifa cha Wanahabari (ICFJ).***

SAYANSI

NA MICHAEL ENEZA

KITISHO MOTO

# Kilimo, radi, kiangazi vyatajwa kuleta balaa



Moto ukiharibu eneo oevu lenye majimaji nchini Indonesia **PICHA: MTANDAO.**

MATAIFA mbalimbali duniani yanaendelea kushangazwa na kuenea kwa moto wakati wa kiangazi na hata msimu wa baridi au kipupwe kikali, kuliko ilivyowahi kutokea miongo ya nyuma.

Shirika la Utangazaji la Uingereza BBC kwa mfano, linaeleza jinsi Indonesia nchi yenye visiwa zaidi ya 1,000 ukanda wa Ikweta huko Mashariki ya Mbali ilikuwa tayari katika 'kipindi cha moto' badala ya msimu wa kiangazi kama ilivyokuwa kawaida.

Shirika la Mazingira na Amani Duniani Greenpeace linasema katika mchanganuo kuwa Siberia, eneo kubwa la mashariki ya Russia ambalo lina viwango vya ubaridi visivyoonekana kokote kwingine, kwa sehemu kubwa imekumbwa na moto huyo.

Kwa baadhi ya wataalamu inashangaza pia kuwa misitu ya Amazon, ambayo ni nyumba ya mito mingi mikubwa mingi inayochangia mtiririko wa mto wa Amazon, pia liko katika moto wakati ni sehemu oevu na tepetepe kwa wingi wa maji.

Inaonyesha kuwa viwango vya joto na kwa hivyo ukame wa ziada maeneo mengi duniani unasababisha moto huyo.

Katika mahojiano na baadhi ya wapambanaji na moto katika jimbo la California pwani ya magharibi ya Marekani, wataalamu wanasema moto wa wakati huu una nguvu mara 10 zaidi ya ilivyokuwa miongo iliyopita. Kwa miaka mingi nyakati za kiangazi ilikuwa ikionekana maeneo yenye kukaribia majangwa na kuleta taabu hasa kwa wahifadhi misitu.

Baadhi ya wakazi wa maeneo ya kifahari jijini Los Angeles Marekani ilibidi wakimbie maskani iliposhindikana kuzima moto usifike jijini.

Taarifa za satellite za kuangalia hali ya hewa za Chuo Kikuu cha Swansea nchini Uingereza zilitumika kuorodhesha idadi ya moto nchini Indonesia tangu mwaka 2002.

Ilionekana kuwa kwa kiasi fulani miaka hii minne iliyopita ilikuwa afueni, kwani mwaka 2015 kulikuwa na moto zaidi ya 75,000 nchini humo, wakati mwaka jana ilikuwa zaidi tu ya 35,000 na pungufu zaidi miaka miwili iliyotangulia.

Kuna vyanzo tofauti vya moto kulingana na utafiti mojawapo kwa mfano nchini Indonesia ni uchomaji wa miti ya zamani (kwa mfano ya mawese ambayo biashara yake ni nzuri) ili kupanda miti mipya.

Moto wa aina hiyo unaweza kusafirishwa na upepo na kuenea kwa mapana na marefu kwani ukame unakausha uoto wa asili na kuuwezesha kupokea moto huku upepo ukiuongezea nguvu.

Kwingineko kuna mabadiliko ya sera yenye lengo kama hilo, kutumia eneo kubwa zaidi kwa mfano misitu ya Amazon kufungua mashamba makubwa, sera mpya huko Brazil.

Kuna takwimu za kushangaza kwa upande wa Brazil kwani idadi ya moto kati ya Januari na Agosti mwaka jana ilikuwa mara mbili ya moto kama hiyo mwaka uliotangulia. Ila wataalamu walipoliganisha takwimu za muda mrefu zaidi waliona kuwa licha ya kuongezeka kwa moto kwa kasi, bado hakujafikia moto wa mwaka 2002 hadi 2010.

Ina maana 'mashambulizi' ya kilimo dhidi ya misitu ya Amazon yalianza kushika kasi mwanzoni mwa karne ya 21 yakatulia kiasi fulani kutokana na upinzani wa jumuiya ya kimataifa.

Hivyo maeneo ya misitu ya Brazil yaliyochomwa kubadilishwa kuwa mashamba yalikuwa makubwa sana katika miaka 10 ya 21, yakapungua kiasi fulani hadi 2015 yalipozidi na hata 2017.

Mwaka juzi na jana maeneo mapya hayakuwa makubwa hivyo kasi ya kupata ardhi ya kufungua mashamba labda imefikia kiwango kinachohitajika na uchomaji misitu unapungua kwa jumla.

Moto ni kama ishara kuwa eneo hilo limeshachukuliwa kwa ajili ya kilimo, kwani miti mikubwa inakatwa, ichomwe kuondoa wanyama waharibifu kuwezesha kilimo na mifugo kuanza. Huwezi kuanzisha shamba bila kulichoma.

> Kuna vyanzo tofauti vya moto kulingana na utafiti mojawapo kwa mfano nchini Indonesia ni uchomaji wa miti ya zamani (kwa mfano ya mawese ambayo biashara yake ni nzuri) ili kupanda miti mipya.

**RADI ZATAJWA**

Ripoti inasema kuna moto ambao hausababishwi na kupanuliwa kwa shughuli za kilimo, kwa mfano moto wa California, Siberia na hata Australia, ukanda wa pwani ya mashariki ambao una uoto mzuri ukilinganisha na maeneo makubwa ya magharibi ambako ni jangwa.

Moto huo mara kadhaa unatokana na radi ambazo zinalipuka wakati wa jua kali, licha ya kuwa wanasayansi ya awali waliambiwa radi ni mgongano wa wimbi la baridi la joto ina maana, hata ingekuwa ni mawimbi makavu.

Moto kama huo kwa jumla umekuwa ukiongezeka Siberia ambalo ni baridi sana, na halina msongamano mkubwa wa kuanzisha mashamba kama ilivyo misitu ya Brazil.

Hali ya ukame imekuwa ikiongezeka na mawimbi ya anga za juu yenye joto kutokea maeneo ya kaskazini ya tropiki hugusa ukanda huo, kuleta radi hizo, wataalamu wanasema.

Taarifa nyingine zinaeleza kuwa satelaiti za shirika la utafiti wa anga za juu la Marekanii (NASA) zinaonyesha kuwa maelfu ya moto umekuwa jambo la kawaida kuanzia mwaka 2003 katika maeneo ya misitu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Angola na Zambia.

Pamoja na kuwa moto huyo haujafikia viwango vikubwa zaidi katika miaka ya karibuni, umekuwa ukipingua kidogo tu hapa na pale kwa kipindi cha miaka 16 iliyopita, 350,000 kwa mwaka 2007 lakini ulikuwa moto 400,000 mwaka 2016 huko DRC.

Baadhi ya wataalamu walijaribu kufananisha moto wa nchi hizo tatu (bonde la mto mkubwa wa Congo) na moto wa Amazon japo wengine wanapiga. Wanasema moto wa Afrika unaendana na hali ya kiangazi ya kutayarisha mashamba kwa ajili ya kilimo, siyo kukata miti ya msitu mnene ili kufungua mashamba makubwa kama ilivyo kwa nchi za Amazon.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

## UN: COVID 19

# Imevuruga utalii, kuharibu ajira, uchumi,urithi wa asili

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, katika tamko lake la kisera kuhusu utalii na COVID-19, amesema janga la corona limeleta maumivu makali kwa kuona jinsi ambavyo utalii umeharibiwa na maradhi hayo yaliyosambaa karibu dunia nzima .

Kiongozi huyo akizungumza kwa njia ya video wiki hii, anasema utalii ni miongoni mwa sekta muhimu zaidi duniani na ni miongoni mwa maeneo yanatoa ajira kwa mtu mmoja katika kila watu 10 duniani kote, huku ikiwapa kipato mamilioni ya watu.

"Inakuza uchumi na kuwezesha nchi kustawi. Inaruhusu watu kuendeleza utajiri wa kitamaduni na asili na kuwaunganisha wanadamu na kuonyesha utu wetu. Kwa kweli, unachoweza kusema ni kuwa utalii wenyewe ni moja ya maajabu ya ulimwengu. Ndio maana imeleta maumivu makali kuona jinsi ambavyo utalii umeharibiwa na janga la COVID-19." Anasema Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Guterres akieleza tathimini ya athari ya COVID-19 kwa utalii anasema kuwa katika miezi mitano ya mwanzo wa mwaka huu wa 2020, zaidi ya nusu ya watalii wanaowasili kimataifa walipungua na hivyo dola bilioni 320 katika mauzo ya nje kutokana na utalii zimepotea.

Aidha, Katibu Mkuu anaeleza kuwa kwa jumla, ajira za moja kwa moja milioni 120 katika utalii ziko hatarini. Wahusika hao wengi wako kwenye sekta za uchumi usio rasmi au katika biashara ndogondogo, ndogo na za kati, ambazo huajiri idadi kubwa ya wanawake na vijana.

"Janga hili ni mshtuko mkubwa kwa uchumi ulioendelea, lakini kwa nchi zinazoendelea ni dharura, hasa kwa mataifa mengi madogo ya visiwani yanayoendelea na nchi za Afrika. Kwa wanawake, jamii za vijijini, watu asilia na watu wengine wengi waliotengwa kihistoria, utalii umekuwa chombo cha kuwaunganisha, kuwawezesha na kutengeneza kipato. Utalii pia ni nguzo muhimu kwa uhifadhi wa urithi wa asili na kitamaduni." Anasisitiza Guterres.

### KUONGEZEKA UJANGILI

Vilevile Katibu Mkuu wa UN, amegusia ujangili alisema kuwa kupungua kwa mapato kumesababisha kuongezeka kwa ujangili na uharibifu wa makazi ya viumbe na kuzunguka maeneo yaliyotengwa na kufungwa kwa sehemu nyingi za urithi wa dunia kumeinyima jamii mapato.

"Ni muhimu kwamba tuijenge tena sekta ya utalii. Lakini lazima iwe katika njia iliyo salama, sawa na rafiki kwa tabianchi." Anashauri Guterres.

Pia, anaeleza kuhusu uchafuzi wa hali ya hewa akieleza kuwa uzalishaji wa gesi ukaa itokanayo na usafirishaji unaweza kuongezeka tena ikiwa ari ya kusimama upya haitolinganishwa na malengo ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.

Guterres anasema kusaidia mamilioni ya watu ambao wanategemea utalii inamaanisha kujenga usafiri endelevu na wenye uwajibikaji ambao ni salama kwa jamii wenyeji, wafanyakazi na wasafiri.

### CHA KUFANYA

Anatoa ushauri ili kuokoa hali hiyo akisema baada ya kueleza namna ambavyo COVID-19 imeuathiri utalii kote duniani na kueleza maeneo matano ambayo ameyaanisha kuwa ni ya muhimu na kipaumbele ili kusaidia hali kurejea na kusimama upya.

Kwanza anasema ni kupunguza athari za kiuchumi na kijamii zitokanazo na janga hili. Aidha, kujenga ustahimilivu katika mnyororo wa thamani kwenye utalii. Halikadhalika anataja kuongeza matumizi ya teknolojia katika tasnia ya utalii.

Katibu Mkuu wa UN, anaeleza jambo la nne kuwa ni kukuza uendelevu na ukuaji imara. Na ya tano, kukuza ushirikiano ili kuwezesha utalii kusaidia zaidi Malengo ya Maendeleo Endelevu.

"Tuhakikishe utalii unarejea tena kwenye nafasi yake kama mtoaji wa ajira, kipato thabiti na ulinzi wa urithi wetu wa kitamaduni na asili." Anaongeza.

Wakati huohuo, Shirika la afya la Umoja wa Mataifa, WHO limesema kuna uwezekano mdogo sana kwa mtu kuambukizwa zaidi ya mara moja ugonjwa wa virusi vya Corona au COVID-19.

AIdha, nchi 172 sasa zinashiriki katika mpango wa kimataifa wa fursa za usoni kwa ajili ya upatikanaji wa chanjo dhidi ya janga la virusi vya corona au COVID-19 ujulikanao kama COVAX, ambao umeundwa ili kuhakikisha fursa sawa za chanjo ya virusi vya corona, WHO ilitangaza wiki hii.

Akitoa tangazo hilo katika mkutano wa waandishi wa habari kwa njia ya mtandao mjini Geneva Uswis , Mkurugenzi Mkuu wa WHO Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus alisema "Nina furaha kubwa kuripoti kwamba hadi kufikia sasa nchi 172 zinashiriki katika mpango wa kimataifa wa huduma ya chanjo COVAX, ambao una mchanganyiko na asilimia kubwa zaidi ya orodha ya chanjo za COVID-19 duniani."

Mpango wa COVAX unaongozwa na muungano wa chanjo duniani GAVI, WHO na muungano kwa ajili ya ubunifu wa kujiandaa na magonjwa ya mlipuko (CEPI), aidha, umeundwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba kuna fursa sawa za upatikanaji wa chanjo ambayo itatengenezwa na kuruhusiwa kutumika duniani.

Hivi sasa ina aina tisa za chanjo za kupambana na COVID-19 ambazo zinauwezekano wa kutumiwa na lengo la COVAX ni kuhakikisha usambazaji na ufikishaji wa dozi bilioni 2 kwa nchi ambazo zitajiunga ifikapo mwisho wa mwaka 2021.

Tedros katika tangazo lake ameongeza kuwa "Hivi sasa chanjo tisa ni sehemu ya orodha hiyo ambayo inafanyiwa tathimini kila wakati na kuhakikiwa ili kuhakikisha fursa ya uwezekano wa kuwa na dawa bora zaidi. Majadiliano tayari yanaendelea na wazalishaji wengine wane. Chanjo zingine 9 hivi sasa zinachunguzwa kwa ajili ya mipango ya muda mrefu."

*UN NEWS*

> "Janga hili ni mshtuko mkubwa kwa uchumi ulioendelea, lakini kwa nchi zinazoendelea ni dharura, hasa kwa mataifa mengi madogo ya visiwani yanayoendelea na nchi za Afrika. Kwa wanawake, jamii za vijijini, watu asilia na watu wengine wengi waliotengwa kihistoria, utalii umekuwa chombo cha kuwaunganisha, kuwawezesha na kutengeneza kipato. Utalii pia ni nguzo muhimu kwa uhifadhi wa urithi wa asili na kitamaduni." Anasisitiza Guterres.



Magofu ya Bagamoyo ni miongoni mwa vivutia watalii duniani. Janga la corona linakwamisha watalii kutembea . **PICHA: MTANDAO**





# Viongozi wa dini wapewa neno kuelekea uchaguzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewataka viongozi wa dini kuhubiri amani katika nyumba za ibada, ili uchaguzi mkuu ufanyike kwa utulivu.

Jafo alisema hayo jana alipokuwa akifungua semina elekezi kwa viongozi wa dini kuhusu masuala ya amani wakati wa uchaguzi mkuu.

Semina hiyo iliandaliwa Taasisi ya Markaz Islaam ya Chang'ombe jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Dodoma.

Akifungua semina hiyo, Waziri Jafo alisema amani ni muhimu wakati wa uchaguzi mkuu ili kuendelea kuifanya Tanzania kuwa kisiwa cha amani.

"Twendeni tukahubiri amani. Hakuna binadamu ambaye aliyekamilika ila lazima tuvumiliane, tupime nia za watu. Tuna kila sababu ya kuendelea kupendana, viongozi wa kisiasa nao wana wajibu wa kuendelea kuhubiri amani," alisema.

**Mataifa yote yanayotuzunguka yote yamepata misukosuko. Ukienda hapo Kongwa unaona kambi tulikuwa tunawalea. Sisi Tanzania tuna wajibu wa kuendelea kulinda amani.**

Jafo alisema Watanzania wanatakiwa kulinda amani wakati wa uchaguzi mkuu na wasikubali uchaguzi huo uwe chanzo cha kuvuruga amani iliyopo.

"Mataifa yote yanayotuzunguka yote yamepata misukosuko. Ukienda hapo Kongwa unaona kambi tulikuwa tunawalea. Sisi Tanzania tuna wajibu wa kuendelea kulinda amani," alisisitiza.

"Bahati mbaya kila mtu ana urefu wa kamba yake. Amani ikiharibika kesho hayupo... mwenzangu na mimi umejitahidi sana umeenda Chemba, mwingine kakimbilia Kondoa, mwenzako ana hati za kusafiria mbili, mambo yakiharibika tu huyo," alisema Jafo.

Pamoja na hayo, Waziri Jafo aliwaomba maimamu wa misikiti kuweka utaratibu wa kuhubiri amani kwa waumini kila ibada ya Ijumaa.

"Agenda ya amani ni msingi wa kila kitu. Tuna siku kadhaa za kwenda katika uchaguzi mkuu. Fursa hii inatakiwa pia kuwapo katika hotuba za maimamu tuwe tunaweka kipengele cha amani," alisema.

"Amani ndiyo jambo kubwa sana katika maisha ya binadamu, wenzetu wanaishi kwa kujificha wengine wanafanya ibada silaha ipo pembeni tena inawezekana wa imani moja. Hakuna jambo linalouma kama familia, kudhalilishwa kama binadamu," aliongeza.

Awali, Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Rajabu, aliwataka mashekhe kuhubiri amani na kutoruhusu nyumba za ibada kutumiwa na wanasiasa kufanya kampeni.

"Niwatake masheikh kuhubiri amani. Amani yetu furaha yetu, tusikubali msikiti wowote kuvunjwa amani. Ukijinasibisha na kundi fulani la kisiasa wewe utakuwa chanzo cha uvunjifu wa amani. Sisi la kwetu ni kuwaelekeza kudumisha amani na kuwagundua wahalifu," alisema.





Dk. Elizabeth Lema (wa pili kulia) wa kampuni ya tiba mbadala ya Cornwell Tanzania, akimpa maelezo mmoja wa wananchi aliyetembelea banda la kampuni hiyo, kwenye Wiki ya Maadhimisho ya Tiba Asili ya Mwafrika Kitaifa yaliyoandaliwa na Wizara ta Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto, jijiji Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Umeme wa REA waleta neema Bahi

**Na Augusta Njoji,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, amesema kwa kipindi cha miaka mitano, vijiji vilivyounganishwa na umeme vimeongezeka kutoka sita hadi 42, hali iliyochochea kasi ya maendeleo ya wilaya.

Akizungumza na Nipashe jana, mkuu huyo alisema vijiji 17 vilivyobaki vitafikiwa na huduma hiyo mwaka huu. Vijiji hivyo ni kati ya vijiji 59 vilivyopo kwenye wilaya hiyo.

Alisema hali hiyo imechangia wananchi kuanzisha miradi na viwanda vidogo ambavyo awali walishindwa kufanya hivyo kutokana na kukosekana kwa umeme.

"Kwa mfano mashine za kusaga nafaka kwa kiwango kikubwa zilikuwa za kutumia mafuta ya dizeli lakini kutokana na huduma ya umeme kufika kwenye maeneo yao, wamebadili na kuanza kufunga zinazotumia umeme. Na hii imechangia pia kuwapunguzia gharama za uendeshaji," alisema.

Kuhusu vitambulisho vya wajasiriamali, mkuu huyo alisema tayari awamu ya pili ya vitambulisho 45,000 vimegaiwa kwa wafanyabiashara hao ili wafanye biashara zao kwenye mazingira rafiki.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Bahi, Dk. Fatma Mganga, alisema kipato cha wananchi wa wilaya hiyo, kimeongezeka kutoka Sh.420, 000 hadi Sh. 980,000.

Alisema hali hiyo imechangia kuongeza mapato ya halmashauri hadi kufikia Sh. bilioni 1.6 kutokana na uwekezaji uliofanywa na kupitia miradi mbalimbali.

Pia alisema uwekezaji kwenye sekta ya elimu katika halmashauri hiyo umesaidia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kutoka wanafunzi 5,000 mwaka 2015 hadi zaidi ya wanafunzi 10,000 kwa mwaka 2020.

"Usajili wa wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza umeongezeka kutoka wanafunzi zaidi ya 1,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi 2,700 kwa mwaka 2020, madarasa 700 yameongezwa kuendana na ongezeko la wanafunzi kupitia mpango wa elimu bila malipo," alisema.

# Mchungaji awataka wananchi wasichague watakaogawa kiitikadi

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Sayuni, Chamwino mkoani Dodoma, Jonas Kabia, amesema katika uchaguzi mkuu mwaka huu, Tanzania haitakiwi kuwapata viongozi watakaowagawa wananchi kiitikadi na kidini.

Mchungaji Kabia aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kawawa wilayani hapa, walioshiriki kwenye maombi maalum kuombea taifa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Alisema Watanzania mategemeo yao makubwa kwenye uchaguzi huo ni kuona wanatumia demokrasia, haki na uhuru katika kuwachagua viongozi wanaowania nafasi hizo za urais, ubunge na udiwani.

Aidha, Mchungaji huyo alisema malengo ya maombi hayo maalumu ni pamoja na kumwomba Mungu ili viongozi watakaochaguliwa watekeleze ahadi ambazo wamezitoa katika kipindi cha kampeni za vyama vyao.

Akizungumza katika maombi hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la AFNET, Sara Mwaga, aliwataka wananchi wenye vitambulisho vya kupiga kura kuvitendea haki kwa kuwapigia kura viongozi watakaoleta maendeleo kwa maslahi ya Watanzania wote.

Pia aliwahamasisha wananchi kuhakikisha hawapotezi haki yao kutokana na kudanganyika kwa kununuliwa chakula, vitenge, fedha na kanga, kwa kuwa hali hiyo itawagharimu kwa kuwachagua viongozi wenye kujali maslahi binafsi.

Alisema wananchi wenye vitambulisho hivyo vya kupiga kura wanatakiwa kutumia haki yao ya msingi, ya kuwachagua viongozi watakaofanikisha kutatua kero bila kujali vyama vyao.

Aliwawata wananchi kuacha tabia ya kubweteka majumbani siku ya upigaji, badala yake wajitokeze watumie haki yao ya kikatiba.

**Wananchi wenye vitambulisho hivyo vya kupiga kura wanatakiwa kutumia haki yao ya msingi, ya kuwachagua viongozi watakaofanikisha kutatua kero bila kujali vyama vyao.**





# Wagombea watakiwa kuweka kipaumbele kuhusu wanawake

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANASIASA walioteuliwa kugombea nafasi za uongozi kuanzia udiwani, ubunge na urais, wameombwa kubeba ajenda ambazo zinalenga kutatua matatizo yanayowakabili wanawake.

Ofisa Programu kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe juu ya masuala ya kuzingatia kwa wagombea katika kipindi cha kampeni hadi uchaguzi mkuu.

Temba alisema wanawake ndilo kundi kubwa la wapigakura nchini, hivyo wagombea wanapaswa kueleza ajenda ambazo zinalenga kulisaidia kundi hilo kwa kuahidi kutatua vikwazo vinavyowakabili.

"Tunategemea kuona kipindi hiki cha kampeni wagombea wote wanapeleka ajenda zinazolenga kuwasaidia wanawake wanapokuwa majukwaani, mfano upatikanaji wa maji kwenye vituo vya afya na makazi ya watu na vifaa tiba vikiwamo vya kujifungulia.

**Vyama vya siasa viwaambie wagombea wao wazungumzie masuala yanayowahusu wanawake hasa wenye mahitaji maalum namna watakavyoweza kutatua matatizo yanayowasibu.**

Kwenye suala ya elimu, wawaahidi wananchi kuboresha mazingira ya shule kwa kujenga mabweni ya wanafunzi wa kike na pedi ili kuwasaidia kumaliza shule, lakini utoaji wa mikopo kutoka halmashauri kwa kuzingatia masharti nafuu," alisema Temba.

Aliwashauri wagombea kuwaeleza wananchi fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye halmashauri sambamba na kuahidi kusimamia programu za uwezeshaji wanawake na vijana kiuchumi kwa kuishauri serikali kuchagua viongozi ambao wana utashi wa kusimamia utekelezaji huo.

Pia alivishauri vyama vya siasa kufuata taratibu za mikutano ya kampeni sambamba na kutengeneza mazingira rafiki kwa wapigakura ili kushiriki mikutano hiyo na kuvutiwa.

Aidha, waendelee kuhubiri amani na mshikamo kwa taifa kwa kuhakikisha mchakato wa kampeni na uchaguzi mkuu unafanyika kwa amani.

"Vyama vya siasa viwaambie wagombea wao wazungumzie masuala yanayowahusu wanawake hasa wenye mahitaji maalum namna watakavyoweza kutatua matatizo yanayowasibu.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, aliwashauri wanawake kote nchini kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili kusimamia na kutekeleza masuala mbalimbali yanayowahusu wanawake.

Alisema idadi kubwa ya wanawake kwenye nafasi za uongozi kuanzia udiwani itasaidia kurahisisha utatuzi wa vikwazo dhidi ya kundi hilo kwa kuhakikisha wanaboresha sera, miongozo na kutoa maoni ya nini kifanyike ili kutengeneza mazingira mazuri.



Mlezi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Mkate, kilichopo eneo la Iwambi, jijini Mbeya, kinachosimamiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde Mbeya, Sista Sabina Siwale (kushoto), akipokea msaada wa chakula kutoka kwa watumishi wa Shule ya Marys ya Uyole jijini humo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Bosi NHIF ataka kikao cha wadau

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga, amemwagiza Mkurugenzi wa Mfuko huo mkoani Mbeya, Mbala Shitindi, kufanya kikao cha pamoja na viongozi wa dini ili kuhamasisha wananchi kukata bima ya afya.

Konga alitoa agizo hilo juzi wakati wa bonanza lililoandaliwa na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya (MZRH), ambalo lilifanyika kwenye viwanja vya Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) jijini hapa. Tamasha hilo lililenga kuwakutanisha watoa huduma za afya na wananchi.

Alisema ni muhimu kukafanyika kikao cha pamoja baina ya viongozi wa nini na NHIF kujadili ni kwa namna gani wataweza kuwahamasisha waumini wao kujiunga na mfuko wa bima ya afya ambao utasaidia kuwa na uhakika wa matibabu.

"Viongozi wa dini wanaongoza kundi kubwa la watu hivyo ni muhimu kufikiwa ili kufahamu ni mbinu gani itatumika katika kuwahamisha watu kukata bima kwa kupitia vikundi, hivyo nakuagiza mkurugenzi wa hapa Mbeya, kaa na hawa viongozi mjadiliane namna gani mtawahamasisha watu kukata bima za afya," alisema Konga.

Aliipongeza Hospitali ya Rufani ya Kanda kwa kuandaa bonanza ambalo limewakutanisha watu wa kada anuai kushiriki michezo ya aina mbalimbali sambamba na wananchi kupima afya zao bure.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Kanda, Dk. Godlove Mbwanji, alisema bonanza hilo limefanyika kwa mara ya tatu sasa na kwamba limefufua matumaini kwa wakazi ndani na nje ya mkoa wa Mbeya kupata fursa ya kupima afya zao bure.

Alisema moja ya mafanikio katika bonanza hilo ni kuongeza marafiki wa hospitali hiyo ambao hutembelea mabanda ya maonyesho kwa lengo la kujifunza na kupata ushauri wa kitabibu kuhusiana na matatizo yanayowasibu.

"Ni miaka mitatu sasa tangu tuanzishe bonanza hili ambalo linahusisha michezo ya aina mbalimbali na upimaji afya bure kwa wananchi wa ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya. Tunajivunia tumesogeza huduma zetu karibu na wananchi lakini pia kuongeza marafiki katika hospitali yetu. Naamini kila mwaka tutakuwa tukiboresha huduma za afya kupitia ushauri unatolewa," alisema Dk. Mbwanji.

# Waanzisha kikundi kuacha utegemezi

**Grace Mwakalinga,** TUKUYU

WANAWAKE wa Kijiji cha Ilalabwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameanzisha miradi ya kiuchumi ikiwamo ya ufugaji na kilimo ili kuwa na kipato endelevu kitakachosaidia kupunguza utegemezi kutoka kwa waume zao.

Wakizungumza na Nipashe jana, wanawake hao ambao wamekubaliana kuanzisha kikundi cha Changamkeni chenye shughuli mbalimbali za kiuchumi, kikiwamo kilimo cha kahawa na migomba, walisema wamepata manufaa makubwa tangu kuanzisha kwake.

Mmoja wa wanawake, Nesi Kasasa, alisema faida alizopata tangu kuanzisha miradi hiyo ni pamoja na kuondokana na utegemezi kwa mume wake na uwezo wa kutunza na kusomesha watoto.

Alisema wanawake hao waliamua kujiunga baada ya kubaini fursa mbalimbali zinazopatikana ndani ya kijiji hicho kupitia kilimo na ufugaji na kwamba waliamua kufanya vibarua kwa ajili ya kukusanya fedha za kununua mashamba na mifugo.

"Wanawake wa kijiji hiki tuliamua kuanzisha miradi kupitia kilimo na mifugo baada ya kupata manyanyaso katika ndoa zetu baadhi yetu walikuwa wanapigwa na kunyanyaswa na waume zao kwa sababu hawafanyi shughuli zozote za uzalishaji na sasa tumeanza kuona manufaa," alisema Kasasa.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Bujesi, Agatha Mwangwego, alisema baada ya kuanzisha miradi ya kilimo na ufugaji, baadhi ya taasisi na mashirika yamevutiwa na kuanza kufanya nao kazi kwa kuwapatia elimu na mikopo ambayo imesaidia kuongeza uzalishaji.

Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), kupitia mradi wa Mwanamke Jasiri, ilitoa mafunzo ya kuwajenga uwezo wanawake hao, kuhusu masuala ya uchumi na uongozi.

Mratibu wa Mradi huo, Theresia Msangazi, alisema wanawake hao ambao waliunda kikundi hicho ni kati ya vikundi 240 vilivyojengewa uwezo katika wilaya nne za Mkoa wa Mbeya kupitia Mradi wa Mwanamke Jasiri.



# TAMWA yashtuka kubakwa kwa mtoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania Zanzibar (TAMWA ZNZ) kimesikitishwa na taarifa iliyotoka hivi karibuni kuwa mtoto wa miaka 12 huko Mwanyanya, mkoa wa Mjini Magharibi, amebakwa mara mbili ndani ya wiki mbili.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa. Alisema baada ya mtoto huyo kubakwa, wazazi wake waliamua kumhamisha kumpeleka Wete, Pemba ambako na huko amebakwa tena.

Dk. Mzuri aliliomba Jeshi la Polisi kuharakakisha hatua za uchunguzi wa kesi hizo ili haki itendeka na kuwataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao kwa muda wote ili kuwalinda na watu waovu.

"Wazazi kuwa karibu na watoto kunatoa ulinzi mzuri kwa watoto na kuwanusuru kufanyiwa ukatili na watu waovu," alisema.

Pia alisema mtoto anapofanyiwa ukatili, wazazi wanatakiwa kuwa makini na kuwa karibu zaidi na watoto wao ili kuwafariji na kuwafundisha mbinu za kujikinga zaidi dhidi ya vitendo viovu.

"Kitendo cha kumhamisha mtoto aliyebakwa kutoka sehemu moja na kumpeleka eneo lingine bila ya uchunguzi na ulinzi wa kina kunaweza kusababisha mtoto akaharibikiwa zaidi kimwili, kiafya na kimaisha," alisema.

Alisema TAMWA inasikitishwa kuendelea kwa vitendo vya ubakaji nchini kote ambavyo vinashamiri kila siku na vinasababisha hofu na madhara kwa watu wanyonge hasa wanawake na watoto.

Kwa mujibu wa taarifa za mitandao ya kupambana na ukatili wa kijinsia Unguja na Pemba kwa kipindi cha miezi sita Januari hadi Juni, matukio 108 ya ukatili wa kijinsia yameripotiwa katika shehia mbali mbali ikiwemo Polisi.

Kati ya matukio hayo, matukio 51 yameripotiwa kuwa ni vitendo vya ubakaji wa watoto chini ya miaka 18.

**Kitendo cha kumhamisha mtoto aliyebakwa kutoka sehemu moja na kumpeleka eneo lingine bila ya uchunguzi na ulinzi wa kina kunaweza kusababisha mtoto akaharibikiwa zaidi kimwili, kiafya na kimaisha.**

# SMZ, Zanlink zaingia mkataba huduma nafuu mawasiliano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA YA Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, imetiliana saini makubaliano ya huduma ya mtandao wa intaneti na kapuni ya Zanlink ili kuwezesha wananchi kupata huduma hiyo kwa bei nafuu.

Makubaliano hayo yalifanyika wizarani hapo, Kisauni, Zanzibar jana mbele ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mustafa Aboud Jumbe na kutiwa saini na Meneja wa Zanlink, Sanjay Raja na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Miundombinu ya Tehema Zanzibar, Mhandisi Shukuru Awadh Suleiman.

Akizungumza katika kikao hicho, Jumbe alisema mawasiliano ya intaneti yamekuwa yakirahisisha shughuli mbalimbali za kibiashara.

Alisema kipindi hiki ambacho baadhi ya mataifa ya nje yanakabiliwa na janga la corona, wafanyabiashara wa Zanzibar wanaagiza bidhaa wanazozihitaji kupitia mawasiliano ya intaneti.

Jumbe alisema mtandao huo umekuwa ukirahisisha maisha ya watu na yanaokoa muda pamoja na kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi.

"Napongeza hatua hii ambayo imepata baraka kutoka serikali na niwatakie kila la heri katika usimamizi na utekelezaji wa mkataba huu," alisema Jumbe.

Naye Suleiman alisema kuwa Zanlink ni wadau wakuu wa miundombinu ya mawasiliano tokea serikali kuanza biashara ya mkonga wa taifa ambao umeondoa changamoto ya mawasiliano ya intaneti.

Aliitaka Zanlink kuiangalia jamii kwa sababu baadhi ya jamii haina mawasiliano ya aina hiyo, hivyo kuunga mawasiliano hayo ya mtandao katika vituo vya tehema kwa jamii ili jamii iweze kufaidika.

Raja kwa upande wake aliipongeza wizara hiyo kwa kuipa fursa kampuni yao kuutumia mkongo wa taifa, hivyo mawasiliano ya intaneti yatawafikia wananchi wengi.

Alisema uchumi wa sasa unategemea mtandao wa intaneti, hivyo wataitumia fursa ya kuwafikia walengwa wengi kuitumia huduma hiyo ili kukuza uchumi.

**uchumi wa sasa unategemea mtandao wa intaneti, hivyo wataitumia fursa ya kuwafikia walengwa wengi kuitumia huduma hiyo ili kukuza uchumi.**




Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar, Mhandisi Shukuri Awadhi (kulia) na Meneja wa kampuni ya Zanlink, Sanjay Raja (kushoto), wakisaini hati ya makubaliano ya huduma ya intaneti, mjini Zanzibar, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# RC ataka kasi ujenzi wa shule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kati kuhakikisha ujenzi wa Shule ya Maandalizi na Msingi Uchukuni, unakamilika ifikapo Januari, mwakani.

Mahmoud aliyasema hayo jana aliposhiriki ujenzi wa taifa wa shule mpya ya maandalizi na msingi katika kijiji cha Uchukuni.

Alisema hatua hiyo itawasaidia wanafunzi wa kijiji hicho kuondokana na adha ya kufuata elimu masafa marefu hali inayosababisha kurejesha nyuma maendeleo ya upatikanaji wa elimu katika kijiji hicho.

Mkuu wa mkoa huyo alisema serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja inaendelea kuchukua jitihada za kusogeza huduma mbalimbali za kijamii zikiwamo maji safi na salama, elimu na barabara itakayoanza ujenzi wake hivi karibuni.

Kadhaika, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuongeza nguvu kazi ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa haraka.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, alisema kukosekana kwa shule katika kijiji hicho, kunasababisha anafunzi hao kukumbwa na matatizo mbalimbali ikiwamo vitendo vya udhalilishaji.

Alisema watoto wanapoenda Shule ambayo hutembea kwa masafa marefu wadhalilishaji hupata mwanya wa kuwavizia watoto hao njiani na kuwafanyia udhalilishaji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA, K**IWANJA CHA COMMERCIAL 1300SQM KINAUZWA KIPO REGENT ESTATE HAKUNA DALALI TUPIGIE: 0693 689996/ 0757 129546

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo ukonga kitunda Mwanagati Ukubwa 3175sqm kandoni mwa barabara kubwa kimepimwa kinafaa kwa shughuli yeyote utakayo ujirani mzuri, Lorry kubwa kinaingia Bei ni 75 mil. Mawasiliano: 0719 619 444/ 0782 574 669


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN JOACHIM MAKABE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0168/0507** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia St. Joseph Seminary Sanu mwaka 2004. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SIN/SIN/RB/630553/2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;222/2020**

**Ombi la (1) SIWEMA ABDULY (2) NEEMA ABDULY,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ABDULY ALLY DIFUGWA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/08/2020.

115878702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**
**Wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI 263/2020**

**Mdai ................................MWARAMI JUMA HAJI**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa........................... SAIMON PETER BINDE WA IPAGALA – DODOMA**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba Madai ya pesa TSH. 48,000,000/=**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 11/09/2020 saa 02.00 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujiteta katika shauri hilo.
Angalia kama *haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama *umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 27/8/2020.

115879702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;241/2020**

**Ombi la OMARY MOHAMED OMARY,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NG'ANZI MOHAMED OMARY.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/08/2020.

115879502

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 82/2020**


**Ombi la BALVINDER SINGH VIRDI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu SATWANT KAUR VIRDI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 4/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo . Tarehe 4/9/2020.

115879402

---

## KUPOTEA KWA CHETI



115879302

**BAKARI RAMADHANI AHAMADI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S1367-0059** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia HALE SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KOR/RB/3668/2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo ya CHAMWINO - MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 80 /2020.**

**Ombi la PHILOMENA SHAYO kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu AGUSTINO STEVEN MASSAWE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 16/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 31/08/2020.

115880202

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 83/2020**

**Ombi la BALVINDER SINGH VIRDI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu JASBIR SINGH VIRDI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 4/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo . Tarehe 4/9/2020.

115879402

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 82/2020**

**Ombi la BALVINDER SINGH VIRDI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu GURCHARAN SINGH VIRDI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 4/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo . Tarehe 4/9/2020.

115879402

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 8/2020**

**Ombi la BALVINDER SINGH VIRDI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu TRISHANRAJ SINGH VIRDI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 4/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo . Tarehe 4/9/2020.

115879402

---

## KUPOTEA KWA CHETI



115878502

**SALEHE AKIDA** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S.0631/0135** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia UMOJA SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/609850/2020.**

---

## TAARIFA YA KUPOTEA KADI YA GARI.

**MSAFIRI OMARY HASSANI** NINATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA **T 661 DJJ** NISSAN PICK UP YENYE JINA NYAMONGO SECONDARY SCHOOL. KWA YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/KJN/RB/62640/2020.**

115878602

---

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**IDD AYUBU PISHOCK** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **NOOTE BOOM - TRAILER** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 386 CHR.** CHASSIS NO **0066571.** YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/631899/2020.**

---


Uza,

Chenye Thamani

Kubwa Kwa Kutangaza

Nasi Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ujerumani yalaani jaribio la uvamizi bungeni

**BERLIN,** Ujerumani

VIONGOZI wa Ujerumani wamelaani jaribio la waandamanaji kuvamia Jengo la Bunge wakati wa maandamano dhidi ya vikwazo vya kuzuia kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona na kusema hatua hiyo haikubaliki.

Baadhi ya waandamanaji hao siku ya Jumamosi walibeba bendera ya zamani ya Ujerumani iliyotumika hadi mwishoni mwa vita vya kwanza vya dunia.

Katika ujumbe kupitia mtandao wa Instagram, Rais wa Ujerumani Frank -Walter Steinmeier alisema kuwa bendera hiyo ni udhalilishaji wa mrengo mkali wa kulia mbele ya Bunge hilo.

Alisema na ni mashambulizi yasiokubalika katika demokrasia ya nchi hiyo na kwamba hawatakubali mienendo hiyo.

Steinmeier alisema kuwa watu wana haki ya kuelezea ghadhabu yao kuhusu vikwazo hivyo vya kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya corona na kuvitilia shaka ikiwa ni pamoja na kufanya maandamano lakini akaongeza kuwa uvumilivu wake unafikia mwisho wakati waandamanaji wanaruhusu kutumiwa na maadui wa demokrasia na wachochezi wa kisiasa.

Wakati huo huo, Naibu Chansela wa Ujerumani, Olaf Scolz alisema kuwa haikubaliki na haiwezi kuvumiliwa, baadhi ya watu wanasimama mbele ya jengo la Bunge la Reishstag.

"Nawashukuru sana maofisa wa polisi walioonesha kujitolea kwao na lazima tufanye kila tuwezalo kuhakikisha matukio kama hayo hayatumiwi tena mbele ya jengo la bunge," alisema.

Katika ujumbe kupitia mtandao wa twitter, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Heiko Maas alisema kuwa bendera ya zamani ya Ujerumani mbele ya jengo la Bunge ni fedheha.

Spika wa Bunge la Ujerumani, Wolfgang Schaeuble, amekashifu vikali matukio hayo na kusema kuwa inawahusu watu wote wakati kundi la wachache la mrengo mkali wa kulia linajaribu kuvamia kiti cha uwakilishi wa watu.

Polisi ilisema kuwa takriban watu elfu 38 hii ikiwa idadi mara mbili zaidi iliyotarajiwa, walikusanyika mjini Berlin siku ya Jumamosi kuandamana dhidi ya vikwazo hivyo ambavyo ni kuvaa barakoa na kuacha mwanya kati ya mtu na mwingine.

Siku ya Alhamisi, Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, na viongozi wengine 16 wa majimbo ya shirikisho la Ujerumani waliidhinisha vikwazo vikali vya kukabiliana na kuenea kwa janga hilo vinavyojumuisha faini ya dola 59 kwa wale watakaopatikana hawajavaa barakoa ambazo ni lazima. **DW**

# Mkosoaji wa serikali ya Rwanda atiwa mbaroni

**KIGALI,** Rwanda

MKOSOAJI wa Serikali ya Rwanda anayeaminika kuwa na makazi Ubelgiji na Marekani, Paul Rusesabagina (66), amekamatwa na kurudishwa nchini humo na kuoneshwa mbele ya vyombo vya habari mjini Kigali.

Kitengo cha kufuatilia wahalifu kilisema anatuhumiwa kuhusika na vitendo vya ugaidi na utekaji vilivyofanywa mwaka 2018 dhidi ya raia Kusini mwa Rwanda.

Akiwa amevaa suti nyeusi, shati nyeupe, tai ya njano na barakoa ya rangi ya bluu, Rusesabagina ameoneshwa mbele ya waandishi wa habari katika hatua iliyowashangaza wengi, maana hakuna aliyekuwa na habari za kukamatwa kwake.

Waandishi wa habari walishikwa na butwaa na bumbuazi alipoingia katika chumba walichokuwamo, akiwa ameambatana na askari polisi watatu.

Msemaji wa Ofisi ya Taifa ya Upelelezi Dk. Thierry Murangira, alisema Rusesabagina alitiwa mbaroni kwa ushirikiano wa kimataifa.

**Rusesabagina anatuhumiwa kuunda na kuongoza chama cha kigaidi pamoja na mtandao wa vyama vya kigaidi ikiwamo MRCD na PDR-Ihumure ambavyo vina shughuli mbalimbali katika ukanda huu na kwingineko.**

"Rusesabagina anatuhumiwa kwa kuunda na kuongoza chama cha kigaidi pamoja na mtandao wa vyama vya kigaidi ikiwamo MRCD na PDR-Ihumure ambavyo vina shughuli mbalimbali katika ukanda huu na kwingineko. Murangira alisema.

"Rusesabagina alikuwa ameweke-wa waranti wa kimataifa ya kumkamata ili sheria ifuate mkondo wake, ajitetee kuhusu makosa makubwa yanayomkabili ikiwamo ugaidi, uchomaji na mauaji yaliyofanywa dhidi ya wananchi wasio na hatia katika mashambulizi yaliyofanywa katika maeneo mbalimbali nchini Rwanda ikiwamo shambulizi la mwezi Juni mwaka 2018 huko Nyaruguru na lile la Nyamagabe lililofanyika mwezi Disemba mwaka 2018."

Murangira amejizuia kutoa maelezo kuhusu nchi aliyokuwamo Ruisesabagina wakati anakamatwa na hata tarehe, akisema utoaji wa taarifa hizo unaweza kupotosha juhudi za upelelezi unaoendelea.

Rusesabagina ni maarufu nchini humo na duniani hasa kupitia filamu ya Hotel Rwanda, iliyochezwa kuhusu mchango wake katika kuwaokoa mamia ya watutsi waliokimbilia katika Hoteli ya Milles Collines iliyokuwa chini ya uongozi wake mwaka 1994 katika kipindi cha mauaji ya kimbari.

Filamu hiyo imempatia tuzo za kimataifa kama mpigania haki huku ikikosolewa na wengine wanaosema imesheheni uongo.

Jina lake limetajwa mara nyingi katika kesi ya Nsabimana Callixte maarufu Sankara, ambaye pia alikamatwa akiwa ugenini na kurudishwa nchini Rwanda mwaka jana akikabiliwa na makosa mengi ikiwamo ugaidi.

Waendesha mashtaka walisema Rusesabagina ndiye aliunda kile walichokitaja kuwa mtandao wa kigaidi wa MRCD ambao tawi lake la kijeshi la FLN lilikiri kufanya mashambulizi Kusini mwa Rwanda mwaka 2018, kwa lengo la kuuangusha utawala wa Rais Paul Kagame ambaye wakosoaji wake wanamtuhumu kutovumilia ukosoaji wa aina yoyote. **DW**



Wanandoa Julio Mora (110) na Waldramina Quinteros (104) waliodumu kwenye ndoa kwa miaka 79 watuzwa na Guiness, wenza hawa walioana kwa siri mwaka 1941, baada ya familia zao kutoidhinisha mahusiano yao. **PICHA: MTANDANO**

# Lebanon kumchagua Waziri Mkuu mpya

**BEIRUT,** Lebanon

RAIS wa Lebanon, Michel Aoun, anatarajiwa kufanya mazungumzo na wabunge kwa lengo la kumteua Waziri Mkuu mpya atakayeiongoza nchi hiyo inayopitia mizozo kadhaa.

Aoun atakutana na makundi kadhaa ya wabunge kujadiliana kuhusu suala hilo. Duru za serikali zinaeleza kuwa balozi wa Lebanon nchini Ujerumani, Mustapha Adib huenda akapewa jukumu la kuunda serikali mpya.

Adib aliteuliwa na Waziri Mkuu wa zamani, Saad Hariri, mkuu wa kundi kubwa bungeni la Waislamu wa madhehubu ya Sunni. Kwa mujibu wa mfumo wa Lebanon, Rais anatakiwa awe mkristo kutoka madhehebu ya Maronite, Waziri mkuu awe muislamu kutoka madhehebu ya Sunni na Spika wa Bunge awe muislamu kutoka kwenye madhehebu ya Shia.

Tangazo hilo limetolewa zaidi ya wiki tatu baada ya Waziri Mkuu, Hassan Diab kujiuzulu kutokana na mlipuko mkubwa uliotokea Beirut na kuwaua zaidi ya watu 180 na kuwajeruhi wengine 6,000. **DW**

# VIDAL AFUNGUKA BARCELONA IMEPOTEZA UTAMBULISHO



**BARCELONA,** Hispania

ARTURO Vidal amesema Barcelona inatakiwa "kubadilisha vitu" kwa sababu utambulisho wao umeachwa nyuma kutokana na mgogoro wa ndani ya klabu, kitu kinachoweza kushuhudia Lionel Messi akiondoka.

Messi aliwasilisha maombi ya kutaka kuondoka na nahodha huyo wa Barca ameripotiwa kuwaniwa na Kocha, Pep Guardiola pale Manchester City kwenye Ligi Kuu England, huku Paris Saint-Germain, Inter na Juventus pia zikuhusishwa naye.

Hiyo imekuja baada ya Barca kupokonywa Kombe la LaLiga na wapinzani wao, Real Madrid na pia kuchapwa kichapo cha mbwa koko cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na Ronald Koeman akachukua mikoba ya Quique Setien ambaye aliteuliwa kuwa kocha hapo Januari.

Na kiungo wa Barca, Vidal amekitaka kikosi kubadilisha mtazamo wao huku presha kubwa ikielekezwa kwa rais, Josep Maria Bartomeu.

"Barcelona imefanya vitu ambavyo havipaswi kufanywa na klabu ya daraja la juu," amesema Vidal katika mahojiano na Daniel Habif kupitia mtandao wa Youtube.

"Mwisho wa siku, unakubaliana na hili unapokutana na timu ambayo haijajipanga, timu ambayo haina morali ya ushindi, na wachezaji wasio na njaa ya kushinda kila taji.

"Utambulisho wa Barcelona umeachwa nyuma, timu inakwenda kiholela tu, mambo yanatakiwa kubadilishwa ili kila kitu kiwe sawa."

## Lewandowski mwanasoka bora wa mwaka Ujerumani

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski ametunukiwa tuzo ya Mchezaji Bora wa mwaka wa Ujerumani baada ya kuwa na msimu wa kuvutia na Bayern Munich.

Fowadi huyo alichaguliwa kwa kupigiwa kura na waandishi wa habari kwa kushirikiana na jarida la michezo la Kicker.

Alipata kura 276 kati ya zilizopigwa na wachezaji wa Bayern walishika nafasi ya kwanza hadi ya tatu kwenye tuzo hizo, huku Thomas Muller akishika nafasi ya pili kwa kupata 54, tano zaidi ya alizopata Joshua Kimmich katika nafasi ya tatu.

Bayern ilimaliza msimu wa 2019-20, kwa kushinda taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Kombe la Ligi, DFB-Pokal, na Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kuifunga Paris Saint-Germain 1-0 kwenye fainali.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 32, alifunga mabao 55 katika mashindano yote msimu huu na kuwa mchezaji wa kwanza ambaye si raia wa Ujerumani kushinda tuzo hiyo tangu Kevin De Bruyne alipoitwaa mwaka 2015 wakati kiungo huyo akicheza pale Wolfsburg.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland baada ya kutwaa tuzo hiyo aliliambia jarida la Kicker: "Najisikia fahari kubwa kwa hili.





# Van de Beek apelekwa United

**AMSTERDAM,** Uholanzi

RAFAEL van der Vaart amesema Donny van de Beek anastahili uhamisho wa kwenda Manchester United wakati akimsifia nyota huyo wa Ajax baada ya kuripotiwa kwamba, anakaribia kutua kule Old Trafford.

United inakaribia kumsajili kiungo Ajax, Van de Beek baada ya kuripotiwa wamefikia makubaliano ya ada na miamba hao wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, ambao walimwacha nje nyota huyo kwenye mchezo wa kirafiki uliochezwa Jumamosi dhidi ya Eintracht Frankfurt.

Van de Beek pia amekuwa akihusishwa na miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona na Real Madrid, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 23 anaonekana anaelekea kwenye Ligi Kuu England kwa ada inayotajwa kuwa ni pauni milioni 40.8.

Nyota wa zamani wa Ajax na Uholanzi, Van der Vaart, ambaye aliichezea Tottenham kwenye Ligi Kuu England, amemsifia Van de Beek.

"Donny anastahili sana uhamisho," amesema Van der Vaart akiiambia NOS. "Amecheza kwa kiwango kikubwa sana kwa Ajax.

"Na Manchester United wanahitaji mchezaji aina yake kwa timu yao. Uhamisho ni mzuri kwa upande wetu pia (watu wa Uholanzi). "Tunamfuata. Anastahili uhamisho."

Van de Beek ni zao la akademi ya kukuza vipaji ya Ajax na amecheza kwa misimu mitano kwenye kikosi cha kwanza, akifikisha mechi 200 alizocheza katika mashindano yote.

# Thiago anaondoka Bayern – Rummenigge

**MUNICH,** Ujerumani

THIAGO Alcantara anaonekana anajipanga kuondoka Bayern Munich na Ofisa Mtendaji Mkuu, Karl-Heinz Rummenigge anatarajia kupokea ofa kwa ajili ya kiungo wake huyo ndani ya siku chache zijazo.

Liverpool imekuwa ikihusishwa zaidi na uhamisho wa Thiago, ingawa Rummenigge alisema wiki hii kwamba, Bayern haijapokea ofa yoyote kutoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England.

Hata hivyo, alipoulizwa kuhusu Thiago katika mahojiano na Welt am Sonntag, Rummenigge alijibu: "Inaonyesha atatuacha.

"Ni muhimu kwake ameonyesha kwamba anaweza kucheza vizuri katika mechi kubwa.

"Linapokuja suala hilo, inatuumiza sisi. Natarajia ofa yake kwa siku chache zijazo."

Thiago aliisaidia Bayern kushinda mataji matatu wakati walipotwaa kombe la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya kocha, Hansi Flick.

Hatakuwa mchezaji wa kwanza wa kimataifa wa Hispania kuondoka hapo kwenye dimba la Allianz Arena kuelekea msimu mpya wa 2020-21.

Mlinzi, Javi Martinez pia anaonekana kuwa njiani kuondoka, huku Rummenigge akithibitisha kwamba Bayern haitamzuia kuondoka.

"Javi anafikiria kuhusu kuondoka. Litakuwa jambo gumu pia kwake kwa sasa," aliongeza kusema Rummenigge.

"Mkataba wake bado una mwaka mmoja na tumeshamwelewesha kwamba hatutamwekea vikwazo vya kuondoka."






# IBRAHIMOVIC AMALIZANA NA AC MILAN

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amebainisha "kila kitu kimemalizwa" kwa upande wake kubakia AC Milan kwa ajili ya msimu mpya.

Awali majaliwa ya mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Sweden yalikuwa hayajulikani, kabla ya Milan kuposti video kwenye ukurasa wao wa Twitter na kuandika Ibrahimovic "amerudi".

"Hatimaye, kila kitu kimemalizwa na naweza kurudi tena sehemu ambayo najihisi nipo nyumbani," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38.

"Sasa, muda wa kufanya kazi kwa bidii. Tunahitaji kujituma.

"Kama nilivyosema sipo hapa kwa bahati tu, nipo hapa kwa ajili ya kupata matokeo na kuisaidia timu, kocha na klabu kuifikisha AC Milan pale inapopaswa kuwapo.

"Tulifanya kila kitu kwa kipindi cha miezi sita iliyopita, lakini hatukushinda chochote. Msimu huu, nipo hapa tangu mwanzo, hivyo tunahitaji kuendeleza kile kitu kizuri tulichokifanya, kufanya kazi kwa bidii na kujitolea kwa malengo."

Ibrahimovic alitarajiwa kubakia hapo kwenye dimba la San Siro baada ya kutoa mchango mkubwa kwa kikosi hicho tangu alipotua Januari, akifunga mabao 11 katika mechi 20 alizocheza kwa kipindi na nusu ya msimu wa 2019-20.

Awali Ibrahimovic alitumia miaka miwili na Milan na alifanikiwa kubeba taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, mwaka 2011.

Alihamia Paris Saint-Germain mwaka uliofuata na baadaye akacheza kule Manchester United na LA Galaxy ya Marekani kabla ya kurudi nchini Italia.

# *Spurs yafanikiwa kumnyakua Doherty*

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur imekamilisha usajili wa mlinzi wa kulia, Matt Doherty kutoka Wolves kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 14.7.


Spurs ilithibitisha Jumapili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa mkataba wa miaka minne na amekabidhiwa jezi namba mbili.

Nyota huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Ireland, Doherty amecheza mechi 50 katika mashindano yote kwenye Ligi Kuu England katika klabu ya Wolves msimu uliopita na amefunga mabao saba.

Tottenham ilikuwa inatafuta mlinzi mpya wa kulia baada ya kumuuza, Kyle Walker-Peters kwenda Southampton na inaonyesha wazi kuwa, Serge Aurier anataka kuondoka.

Doherty amekuwa kwenye vitabu vya Wolves kwa miaka 10, akianza kuichezea klabu hiyo kwenye madaraja ya chini.

Ujio wake umezidi kuongeza nguvu kwa Tottenham ambao pia wamefanya usajili wa kiungo, Pierre-Emile Hojbjerg na golikipa, Joe Hart kipindi hiki cha dirisha la usajili.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR RASMI ATABAKIA PSG

## ●●● Afunguka anataka kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuweka historia...

**PARIS,** Ufaransa

MCHEZAJI nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar amethibitisha atabakia katika klabu hiyo kwa ajili ya msimu ujao.

**Mshambuliaji huyo Mbrazili alionekana akitokwa na machozi baada ya mabingwa hao wa Ligue 1 walipopoteza mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich iliyochezwa jijini Lisbon mapema mwezi uliopita.**

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 alikuwa akihusishwa zaidi kurejea katika klabu yake ya zamani ya Barcelona kabla ya likizo ya muda mrefu iliyosababishwa na ugonjwa wa corona (COVID-19).

Lakini Neymar sasa hajawasilisha maombi yoyote ya kutaka kuondoka PSG baada ya kulieleza gazeti rasmi la klabu hiyo yenye mashabiki wengi Ulaya anahitaji kuwa na kipindi kingine kizuri kwenye msimu mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na vile vile kuwa mmoja wa wachezaji wakongwe wa timu hiyo.

"Nitabakia hapa PSG katika msimu ujao! Na nikiwa na malengo ya kucheza tena fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na wakati huu tukiibuka washindi," alisema Neymar.

"Nimefurahishwa na wazo la kufanya kila linalowezekana ili kuacha jina langu kwenye vitabu vya historia ya klabu yangu."

Taarifa mbalimbali zilizopatikana nchini Ufaransa zinaeleza mshambuliaji huyo alikuwa ameshaanza mchakato wa kuhakikisha mchezaji mwenzake wa zamani, Lionel Messi anatua klabuni hapo baada ya nyota huyo kueleza anajipanga kuondoka Barcelona.

Wiki iliyopita, Messi aliandika katika akaunti yake kwa wakongwe wa Catalunya akielezea uamuzi wake wa kushtua wa kutaka kuondoka klabuni huku Manchester City ikionekana kuongoza kwenye mbio za kumsajili wakati klabu hiyo ya Ufaransa pia ikipambana kunasa pia saini ya nyota huyo wa Argentina.

Taarifa hiyo ilikuja siku moja baada ya Neymar kufanya uamuzi wa kusitisha mkataba wake wenye thamani ya pauni milioni 78.6 na Kampuni ya Nike ambao ulidumu kwa miaka 15.

Uamuzi wa Neymar kukata mawasiliano na kampuni hiyo ilikuwa ni habari mbaya kwa PSG, ambao wanatumia vifaa vya michezo vinavyozalishwa na Nike.

Habari nyingine zinasema mshambuliaji huyo anajiandaa kusaini mkataba na Kampuni ya Ujerumani ya Puma, ambao ndio wasambazaji wapya wa vifaa vya michezo wa Manchester City na AC Milan.

Nike imekuwa ikimdhamini Mbrazili huyo tangu akiwa na umri wa miaka 13, muda mrefu kabla ya nyota huyo hajajiunga na soka la kulipwa.

## ZISIKUPITE

### UNITED, VILLA WATETA

MANCHESTER United inaendelea na mazungumzo na Aston Villa kwa ajili ya kuhakikisha wanafikia makubaliano ya usajili wa kiungo mchezeshaji, Jack Grealish, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Mail)***

### SPURS KUIBANA UNITED

TOTTENHAM imejitosa kupambana na Manchester United katika kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Uholanzi na Ajax, Donny van de Beek (23). ***(Mirror)***

### MARTINEZ KUBAKI ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kumpa mkataba mpya golikipa wa Timu ya Taifa ya Argentina, Emiliano Martinez (27), sambamba na beki raia wa England, Ainsley Maitland-Niles (23), kama atakubali kubakia klabuni hapo. ***(Mirror)***

### ARRIZABALAGA: SIONDOKI

GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Hispania, Kepa Arrizabalaga (25), ambaye alikuwa anahusishwa na mpango wa kuondoka Chelsea, amesema anataka kubakia Stamford Bridge na atapambana kuwania namba kwenye kikosi cha kwanza cha klabu hiyo. ***(Sun)***

### RODRIGO ANUKIA LEEDS

LEEDS United imeweka wazi inataka kumsajili kiungo wa Udinese na Timu ya Taifa ya Argentina, Rodrigo de Paul lakini klabu hiyo imesema ili kukamilisha uhamisho wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 26, inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 31. ***(Guardian)***

### SPURS, NEWCASTLE VITANI

TOTTENHAM na Newcastle zimeonyesha nia ya kusaka saini ya mshambuliaji wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Norway, Joshua King, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Chronicle)***

### VIDAL KUREJEA JUVENTUS

KIUNGO wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Chile, Arturo Vidal (33), anatarajia kuwa huru kurejea katika klabu yake ya zamani ya Juventus. ***(Goal)***

### CONTE AMTAKA KANTE

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte anataka kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Chelsea, N'Golo Kante, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Football Italia)***

### PALMIERI ANUKIA INTER

WAKALA wa Emerson Palmieri ameweka wazi Inter inahitaji kunasa saini ya beki huyo wa kulia wa Timu ya Taifa ya Italia ambaye ana umri wa miaka 26 akitokea Chelsea. ***(Goal)***

### HALLER AIKATAA HERTHA

STRAIKA wa West Ham Mfaransa, Sebastien Haller (26), amekataa ofa ya kujiunga na klabu ya Hertha BSC ya nchini Ujerumani. ***(90 mins)***

### SUAREZ KUIKAMUA BARCA

BARCELONA italazimika kulipa kiasi cha pauni milioni 12 kama itahitaji kuvunja mkataba wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Luis Suarez (33), ambaye anaitumikia klabu hiyo. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## TK Master: Bado sijaanza kazi

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya kuonyesha makali katika mchezo wake wa kwanza kwenye mchezo wa kirafiki wa kilele cha Wiki ya Wananchi, winga mpya wa Yanga, Tuisila Kisinda 'TK Master' amesema bado kuna mambo 'makubwa' yanakuja, hivyo mashabiki watulie.

Mbali na uwezo mzuri aliouonyesha, nyota huyo juzi alifunga bao la kwanza katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Eagle Noir ya Burundi, akipokea pasi ya kiungo, Feisal Salum 'Feitoto'.

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi baada ya mchezo huo, Kisinda alisema yeye na wachezaji wenzake wa kigeni wana deni la kuwalipa mashabiki wa Yanga kutokana na hamasa waliyoionyesha tangu walipotua nchini na juzi walipoujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Nimependa hali ilivyokuwa uwanjani, bado naamini kuna mengi ya kuifanyia klabu hii, nawashukuru sana mashabiki tangu siku ya kwanza nilipofika hapa nchini mpaka kwenye mchezo huu," alisema TK Master.

Nyota huyo aliyesajiliwa kwa pamoja na Mukoko Tonombe alisema yupo tayari kwa 'mikiki' ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza mwishoni mwa wiki. Bao lingine la Yanga katika mchezo huo wa kirafiki lilifungwa na Michael Sarpong.

Yanga inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuanza msimu mpya kwa kuikaribisha Tanzania Prisons ya Mbeya, mchezo utakaofanyika Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

## Kiba kuongoza kampeni Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

ZAIDI wa wasanii 100 wa muziki wa kizazi kipya wakiongozwa na mkongwe, Ali Kiba wanatarajia kushiriki katika uzinduzi wa kampeni za mgombea ubunge wa Jimbo la Muheza, jijini Tanga, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' zitakazofanyika kesho kwenye Uwanja wa Jitegemee.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Muheza, Mohamed Moyo, alisema kuwa maandalizi ya uzinduzi huo yamekamilika na anawaomba wanachama na wafuasi wa mgombea huyo kujitokeza kwa wingi kwenye mkutano huo.

"Tunatarajia kufanya uzinduzi wa kampeni zetu Septemba 2, tutakuwa na wasanii zaidi ya 100 ambao watawasili Muheza wakitokea mkoani Dodoma walipokuwa wamekwenda kumuunga mkono Rais John Magufuli katika uzinduzi wa kampeni ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu," alisema Moyo.

Alisema wanatarajia kuwa na maandamano yatakayowahusisha waendesha pikipiki, magari na watembea kwa miguu ambayo yataanza saa 12 asubuhi yakitokea sehemu mbalimbali wilayani hapa na kuelekea kwenye Uwanja wa Jitegemee.

Naye Katibu Mwenezi wa CCM, Wilaya ya Muheza, Sufiani Mwedi, amewataka wanachama wote wa chama hicho kushiriki kikamilifu kwenye uzinduzi wa kampeni hizo na baadaye kwenye mikutano itakayoandaliwa.

# ZLATKO AHITAJI MUDA KUISUKA VEMA YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Yanga, Zlatko Krmpotic, amesema kikosi chake kina wachezaji wazuri, lakini anahitaji kupata muda zaidi wa kuwanoa ili kukijenga imara na kutengeneza muunganiko mzuri.

**Zlatko amesema hayo baada ya kushuhudia kikosi hicho kikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Aigle Noir kutoka Burundi katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam juzi, Zlatko alisema ameona viwango vya wachezaji wake na anaamini akipata muda wa kutosha nyota hao watakuwa na muunganiko mzuri na watafanya vizuri katika msimu ujao.

Kocha huyo alisema licha ya kutokuwa na muda mrefu, atajipanga kuhakikisha anawapa wachezaji wake mazoezi ambayo yatawajenga na wataelewana kwa haraka.

"Wachezaji wote ni wazuri na wameonyesha kiwango kizuri, ila bado muunganiko na mambo madogo ya kurekebisha, ingawa hatuna muda kwa sasa ila tutahakikisha tunatumia muda uliobakia kujenga kikosi imara zaidi," alisema kocha huyo.

Aliongeza pia atahakikisha anaimarisha nidhamu na wachezaji kupenda kujituma ili kila mmoja afikie malengo ambayo yanatarajiwa na klabu hiyo.

"Wachezaji wote ni wazuri na watalеta ushindani mkubwa, hivyo kila mmoja anahitaji kufanya vizuri ili kunishawishi kupata nafasi ndani ya kikosi," alisema Zlatko.

Wakati huo huo bao la kichwa lililofungwa na mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Michael Sarpong limewakumbusha mashabiki wa Yanga ubora uliokuwa unaonyeshwa na aliyekuwa meneja wao, Abeid Mziba wakati akiitumikia klabu yao.

Sarpong alifunga bao la pili dakika ya 59 kwa kichwa 'kikali' kutoka umbali wa mita sita akimalizia krosi 'maridhawa' iliyopigwa na Ditram Nchimbi.

Zlatko kwa kushirikiana na Juma Mwambusi wataiongoza Yanga katika msimu mpya wa 2020/21, ambapo watafungua pazia Jumapili kwa kuwakaribisha Tanzania Prisona wakati mabingwa Simba watakuwa ugenini Iringa wakiikabili Ihefu FC.



Mwakilishi wa Kampuni ya Vodacom, ambao ni wadhamini wakuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Rehema Kipanga (katikati), akimkabidhi medali ya ushindi wa pili mchezaji wa Namungo, Jamal Dullazi, baada ya mchezo wa Ngao ya Jamii uliofanyika kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha juzi. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Mlandege kusajili wachezaji wanne*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, Mlandege FC wamesema wanatarajia kusajili wachezaji wapya wanne ili kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu mpya wa 2020/21, imefahamika.

Katibu wa Mlandege FC, Salum Mohamed, alisema wachezaji hao watakaosajiliwa ni wale watakaokuwa na uwezo wa kuisaidia timu hiyo kufanya vizuri katika msimu mpya pamoja na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mohamed alisema watasajili wachezaji kutoka kwenye klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Ligi Daraja la Kwanza Kanda na wanaamini watanasa nyota wanaowahitaji katika kutimiza malengo yao.

"Mlandege tutasajili wachezaji wazuri kuendana na timu yetu, msimu uliopita tumefanya vizuri hadi tumekuwa bingwa, lakini msimu huu naamini tutafanya vizuri zaidi, tutasajili wachezaji ambao watakuwa chaguo la mwalimu wetu," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza klabu hiyo pia itatoa baraka kwa wachezaji ambao watahitaji kuhama na kwenda kujiunga na timu nyingine.

Wakati huo huo, Kamati ya Waamuzi wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), inatarajia kuendesha mafunzo ya waamuzi wapya kwa ajili ya kuchezesha kwenye msimu mpya wa 2020/21.

Katibu wa kamati hiyo ambaye Kamishna wa Kimataifa wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Muhsini Ali Kamara, alisema mafunzo hayo yanalenga kuongeza idadi ya waamuzi na anawahasisha waamuzi vijana kushiriki mafunzo hayo.

# Michezo



Jumanne Septemba 1, 2020

Nipashe

Neymar rasmi atabakia PSG UKURASA 22

# Kocha Sven akunwa na majembe Yanga SC

●●● Atabiri mbio ngumu za ubingwa, akisifu kikosi chake kucheza kitimu zaidi huku...

**Na Isaac Kijoti,** ARUSHA

LICHA ya kukaribisha msimu mpya wa 2020/21 kwa kutwaa Ngao ya Jamii juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck (pichani), amesifu usajili mzuri uliofanywa na watani zao, Yanga na kutabiri Ligi Kuu msimu huu itakuwa ngumu.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini hapa, ambayo ilikuwa maalum kwa kukaribisha msimu mpya, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Namungo FC kutoka Lindi.**

Shukrani kwa ushindi huo zikimwendea winga Mghana, Bernard Morrison aliyefunga moja na kusababisha penalti iliyozamishwa kimyani na nahodha, John Bocco.

Hata hivyo, baada ya mechi hiyo kumalizika, Sven alisifu namna kikosi chake kilivyocheza kwa ushirikiano mkubwa jambo ambalo lilichangia kuibuka na ushindi huo.

"Ushindi huu ni kuhusu wachezaji kucheza kwa ushirikiano mkubwa na si mchezaji mmoja mmoja, wameshambulia kwa pamoja na kuzuia kwa pamoja," Sven alisema.



"Tumekuwa na muda mfupi wa kujiandaa pamoja, lakini wachezaji wameonekana kuelewana vizuri ninaamini tutaendelea kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano mengine."

Kuhusu mbio za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu, Sven alisema ligi hiyo itakuwa ngumu kwa kuwa timu zinaonekana kujiandaa vizuri hususan katika usajili.

Alipoulizwa kuhusu Yanga, Sven alisema: "Yanga imefanya usajili mzuri, kutakuwa na changamoto kubwa ya ubingwa".

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Namungo FC, Mrundi Thierry Hitimana, alikubaliana na matokeo hayo na kuahidi kurudi kukiandaa vema kikosi chake.

"Hatuwezi kusingizia uchovu, hiyo haiwezi kuwa sababu ya kupoteza, Simba ni timu nzuri na wamecheza kwa kuelewana.

"Hatujakaa pamoja kwa muda mrefu, tunarudi kujipanga na ninaamini ligi itakavyokuwa inaendelea tutazidi kuimarika kuelekea michuano ya kimataifa," alisema Hitimana.

Msimu ujao katika michuano ya kimataifa, Simba itapeperusha bendera ya nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Namungo itabeba dhamana hiyo upande wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa upande wa Ligi Kuu, ambayo itaanza rasmi Jumapili wiki hii, Simba itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa kuivaa Ihefu FC, wakati Namungo ikianzia nyumbani kwenye Uwanja wa Majaliwa ikiwakaribisha Coastal Union, huku Yanga ikiwa mwenyeji wa Tanzania Prisons katika Uwanja wa Mkapa.




Mshambuliaji mpya wa kimataifa wa Yanga kutoka Burkinafaso, Yacouba Sogne (kulia), akiwa na Balozi wa Kampuni ya GSM na msanii maarufu wa muziki wa kizazi kipya, Harmonize muda mfupi baada ya kuwasili nchini. **PICHA: MTANDAO**

## Sogne awasili, aahidi furaha

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI mpya wa Yanga, Yacouba Sogne amesema anafurahi kujiunga na timu hiyo na anaamini atapambana kuhakikisha anafanya vizuri ili kufikia malengo yanayotarajiwa na mashabiki wa klabu hiyo.

Sogne alisema hayo jana mchana baada ya kuwasili nchini akitokea Burkinafaso na kusaini mkataba wa miaka miwili.

"Nimefurahi kuona mapokezi makubwa ya mashabiki, lakini kuja kuichezea timu ya Yanga na kuhakikisha tunafikia malengo yanayotarajiwa," alisema Sogne.

Naye Mkurugezi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Hersi Saidi, alisema nyota huyo amewasili ili kuja kuitumikia Yanga na sababu za kuchelewa zilitokana na kuwa nje ya uwezo wao.

"Tayari mchezaji huyu ni mali yetu, yupo tayari kuitumikia timu yetu kwa muda wote atakapokuwa katika klabu yetu," alisema Hersi. Nyota huyo wa zamani wa Asante Kotoko alitua nchini jana saa 7: 20 mchana kwa ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia ikitokea Addis Ababa akiwa ni mchezaji huru.

Sogne anaungana na wachezaji wengine wa kigeni wapya ambao ni Carlinhos, Michael Sarpong, Tusila Kisinda na Tunombe Mukoko ambao juzi walikuwa ni sehemu ya utambulisho katika sherehe za Siku ya Wananchi.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042